

Language L.14

# Swahili



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

لتعريف بالإسلام

Version Date: 2025



Part of the







Learn more about Islam with our informative and educational materials, translated to over 50+ languages

@islamicicdx



CONTENTS



سبيلك للسلام  
Your Path To Peace...  
**FREE COPY**



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

# UTANGULIZI MFUPI KUHUSU UISLAMU

SWAHILI [01/10]

نبذة عن الإسلام

*Kujifunza misingi  
ya Uislamu*

PART OF



icelibrary.com | islamic.com



دائرة الشؤون الإسلامية والعمل الخيري | Islamic Affairs & Charitable Activities Department (2017/139)

# KUHUSU UISLAMU

Uislamu ni mfumo ulioenea na njia kamilifu ya maisha. Unamuhimiza mtu kuyafanya mafungamano Yake na Allah na viumbe Wake kuwa mazuri. Unamfunza ya kwamba mtu hawezi kupata furaha ya kweli na usalama wa ndani isipokuwa kwa kumtambua Allah, kutendea matendo mema Aliyoyaweka na ambayo manufaa yake yanamrejelea mtu mwenyewe na vilevile jamii yake.

Uislamu ni katika dini zilizo na wafuasi wengi ulimwenguni. Waislamu wako takriban moja ya tano ya idadi ya watu duniani. Kumuamini na kumuabudu Allah peke yake ndilo lengo kuu la maisha haya na la misingi ya Uislamu.

Neno “Uislamu” katika lugha ya kiarabu maana yake ni “kunyenyekaa” na “kujisalimisha” kwa Allah Mmoja. Ambaye ananyenyekaa kwa kutaka kwake hali ya kumtii Allah anaitwa kuwa ni muislamu. Haijalishi kitu ni ipi rangi yake, jinsia yake na asli yake.

Miongoni mwa mambo yanayotofautisha Uislamu na dini zengine ni kuwa haujinasibishi kwa kabila au kwa mtu.

*Waan Islamummaa  
Amantilee bira irra  
Addbaasu keessaa;  
Amantiin Islaamummaa  
Goso tokotti takki  
nama dhuunfaatti  
hinbeekamu.*

## NGUZO ZA IMANI NI SITA

### 1. Kumuamini Allah

Allah ni jina la kibinafsi la muabudiwa wa haki ambaye ni Mmoja.







Allah ni jina la kipekee la kiarabu la mungu mmoja wa haki. Allah hana washirika, wenza, wasaidizi, wazazi wala watoto. Hakuna kitu kinachofanana Naye - Naye ni mwenye kusikia na mwenye kuona yote. Hashirikiani na yeyote katika sifa yoyote ile ya kiungu na kamilifu. Ana majina mazuri kabisa na sifa kuu. Yeye ndiye Aliye juu, Mwenye nguvu, mwadilifu, Mwenye hekima na mjuzi wa yote.







Yeye ndiye kaumba kila kitu na mwenye kukiruzuku. Ametutunuku kwa neema zisizodhibitiwa. Mfano wa neema hizo ni kama kusikia, kuona, kufikiria, kutembea, kuongea, uwezo wa kuzalisha [vitu mbalimbali]. Inatupaswa kwetu kumshukuru na kumuabudu Yeye peke yake hali ya kuwa hana mshirika. Hilo linakuwa kwa kufuata maamrisha Yake na kujiepusha na makatazo Yake.

Ni jambo lisilowezekana kiakili kuhitimisha kuwa ulimwengu huu ulopangika umepatikana wenyewe isipokuwa [kauumba] Yule mwenye hekima, muumbaji na muweza. Kwa ajili hiyo ni jambo lisiloingia akilini ya kwamba utakuwa umejumba wenyewe au ilikuwa ni matokeo yaliyotokea kwa bahati mbaya.

### 2. Kuamini Malaika

Malaika ni viumbe vilivyoubwa kwa nuru, hawamuasi Allah kwa yale anayowaamrisha na wanafanya yale Anayowaamrisha. Tumejuzwa khabari zao baadhi yao, kama vile Jibrili, ambaye kazi yake ni kuwateremshia Mitume wa Allah Wahyi kutoka mbinguni. Mwingine ni malaika wa kutoa roho.





### 3. Kuamini vitabu

Allah kawateremshia Mitume wake Wahyi ikiwa ni uongofu na rehema kwa watu. Kuamini vitabu kunajumuisha kuamini Tawrati na Injili vilivyoteremshwa kwa Musa na Isa. Qur'aan imeteremshwa kwa Muhammad (swalla Allahu 'alayhim wa sallam)

Qur'aan ni maneno ya Allah ambayo ndio Wahyi wa mwisho uliyoteremkia watu wa ardhini kutoka mbinguni. Ndani yake mna alama na miujiza mingi ya wazi yenye kuthibitisha kuwa Qur'aan ni yenye kutoka kwa Allah. Mfano wa yaliyomo:



- Ndani yake mna Ujumbe wa wazi na ulio msafi wa kilimwengu unaozungumzisha asili ya mtu kuhusu kumuamini Allah.
- Ndani yake mna mitindo ilio na lugha za kipekee zinazojulikana na walimwengu watu wa balagha na wasomi wa kiarabu - pamoja na kuwa Aliiteremsha Qur'aan kwa Muhammad ambaye alikuwa si msomi kabisa.
- Ndani yake mna ukweli wa mambo mengi ya kisayansi ambayo yalikuwa hayajulikana na watu katika kipindi hicho - pamoja na kuwa Qur'aan iliteremshwa miaka 1400 iliyopita.
- Qur'aan imelindwa neno kwa neno tangu hapo ilipoteremshwa kwa lugha yake ya kiarabu ya asli. Hili ni tofauti na vitabu vingine ambavyo vimepotoshwa, kubadilishwa au kupotezwa kabisa. Katika maajabu mengine ya Qur'aan ni kuwa hakuna aya hata moja ilio na kosa au hii inaongozile.







Tafsiri/maelezo mengi ya kiakili ya pande zake nyingi za kipekee na miujiza ya Qur'aan yanafahamisha kuwa ni yenye kutoka kwa Allah. Sambamba pamoja na maneno na vitendo vya Mtume (swalla Allahu 'alayhi wa sallam) vilivyo na mnyororo sahihi ndivyo vyanzo na misingi ya Uislamu.

### 4. Kuwaamini Mitume

Waislamu wanaamini kuwa Allah alituma maelfu ya Mitume, angalau katika kila umma alituma Mtume mmoja, wote wakifikisha ujumbe mmoja wa kumuabudu Allah peke yake na kufuata uongofu wake. Miongoni mwa Mitume hao ni Adam, Nuhu, Ibrahim, Daudi, Yusuf, Musa, Isa na Muhammad (swalla Allahu 'alayhim wa sallam). Kazi yao kubwa ilikuwa kuwalingania watu kumuabudu Allah Pekee na wao wawe ni viigizo vyema vya kuigwa katika kumuabudu Allah na kuwaongoza watu katika njia takasifu. Hakuna Mtume yeyote anayeshirikiana na Allah kwenye chochote katika uungu, uola au kuwafanyia ibadah yoyote, au kumuabudu Allah kupitia wao, kitendo hichi kinabomoa msingi wa Tawhid ambayo ndio haki ya Allah juu ya viumbe.

### Mtume Isa

Waislamu wanaamini kuwa Isa ni Mtume mtukufu wa Allah, ambaye alizaliwa na mama yake bikra Mariam bila ya kuwa na baba. Allah alipitisha miujiza mingi kupitia kwake kwa idhini Yake, kama kumfanya kipofu akawa anaona, kiziwi kusikia, mgonjwa kupona, alizungumza akiwa mtoto mchanga akimtetee mama yake tuhuma alizotupiwa. Pamoja



na kuwa waislamu wanamtukuza na kumpenda Isa, hawamuabudu. Vilevile hawamzingatii kuwa ni mwana wa Allah - Ametakasika Allah kutokana na imani ya utatu. Vilevile hashirikiana na Allah katika sifa yoyote ile ya uungu ambayo amepwekeka nayo.

*“Haiwi kwa Allah ajichukulie mwana yeyote. Utakasifu ni Wake! Anapohukumu jambo basi huliambia: “Kuwa! na linakuwa.”*

Qur'aan 19:35

## Mtume Muhammad

Mtume Muhammad (Swalla Allahu 'alayhi wa sallam) ndio Mtume wa mwisho. Ametumwa kwa uongofu na dini ya haki kwa walimwengu. Allah amemteremshia Qur'aan ambapo Mtume akaifasiri kwa maneno, matendo na hali zake ambapo ikawa wazi kabisa. Mtume alikuwa ni kiigizo chema katika amana, huruma, ukweli na ushujaa. Kama ulivyo msimamo wa waislamu kwa Isa, vivyo hivyo hawamuabudu Muhammad (swalla Allahu 'alayhi wa sallam).

## 5. Kuamini siku ya mwisho

Siku ya mwisho ni lazima itokee na ni miadi ambayo haikwepeki. Siku ambayo viumbe wote watasimama mbele ya Mola wao ambapo atawauliza na kuwafanyia hesabu juu ya matendo yao yote, makubwa na madogo, mazuri na mabaya.

Katika siku hii kuu Allah kwa uadilifu na hikma Yake atayasawazisha mambo yote na hakuna nafsi yoyote ile itayodhulumiwa hata punje kidogo. Watiifu watalipwa na kusaidiwa, na watenda dhambi wataadhibiwa na kula khasara. Wote watahukumwiwa kwa uadilifu na huruma wa Allah, ima wataingia motoni kwa uadilifu Wake au peponi kwa upole na huruma wake.

Kusingelikuwa siku ya malipo (siku ya kiyama), basi maisha yangelikuwa na kudhulumiana sana - ametakasika Allah kutokamana na hilo.

## 6. Kuamini Qadar

Allah anayajua yote yaliyokuwepo, yatayokuwepo na yasiyopo lau yangekuwepo namna yangevyokuwa. Mikononi Mwake kuna uendeshaji wa kila kitu - hakuna kinachopitika katika ulimwengu huu bila ya ujuzi, idhini, hikma na uwezo Wake.

Allah amempa kila mmoja uhuru wa kuchagua lililo zuri na baya, halafu atawahesabu kwa chaguo hili ambapo ima ataingia peponi au motoni.

Hakuna ukinzani baina ya uhuru wa kuchagua na ueneaji wa ujuzi wa Allah wa kutokea kwa mambo na kuyaidhinisha. Haina maana pia kwamba ueneaji wa uwezo wa Allah juu ya kila kitu unaathiri kitu pendekezo huru la mtu. Haina maana vilevile ujuzi wa Allah juu ya pendekezo huru la mtu ni kuwatenza nguvu kwa chaguo hili. Kama ambavyo haina maana kwamba Allah anapenda kila anachofanya kitokee.

*Guyyaan Murtii kun osoo jiraachuu dhabee, jiruun silaa haqan turre, waan duniyaa kanarratti hundi namaa wal qixa haqaan hin tajaajilamneef, murtii haqaas duniyaa kanarratti waan hundi argataa hin jirreef jecha.*

# NGUZO 5 ZA IBADAH

## Nguzo tano za maisha ya muislamu

### 1. Kuamini

Kukubali kumuamini Allah kunakuwa kwa kushuhudia ya kwamba hapana mungu anayeabudiwa kwa haki ila Allah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah.


Shahada hii inatakiwa itokamane na moyo wenye imani ya kweli, kuwa na nia safi kwa Allah, kuitamka na kutenda kazi kwa mujibu wake. Kwa shahada hii mtu anakuwa amekufuru waungu wote wanaobudiwa badala ya Allah na sambamba na hilo anathibitisha kuwa Allah peke ndiye mungu wa kweli na vingine vyote vinavyoabudiwa badala yake ni batili na kwamba Muhammad ndiye Mtume wa mwisho - kwa hayo ndio mtu anakuwa muislamu.

### 2. Kusali sala tano

Sala inazalisha uhusiano wa kinafsi na wa kiroho kati ya muislamu na muumba Wake, na inakumbushia uwajibu wa mtu alionao wa kumtii Allah.

Sala tano ndio nguzo kubwa katika Uislamu baada ya shahada.

Kila sala inaweza kusaliwa wakati na dakika ndogo tu, kunasomwa Qur'aan, kumuomba Allah, kumsifu na kumtukuzua. Muislamu anapojiandaa kwa ajili ya swalah, anatakiwa kuhakikisha ameosha baadhi ya viungo maalumu kwenye mwili wake, kama mfano wa uso na mikono miwili, ili kupatikane usafi wa kiroho na wa kimwili.



### 3. Zaka







Zaka ni faradhi iliyofaradhiwa na Allah juu ya mali ya kila muislamu iliyofikisha kiwango fulani inayotolewa kwa njia maalumu.







Kunatolewa takriban 2.5% ya mali iliyopitikiwa na mwaka kupewa watu wenye kustahiki, kama mfano wa mafukara, maskini na wengineo. Zaka inaisafisha mali ya mtu na inapelekea katika manufaa mengi kwa yule mtowaji na mpewaji. Katika manufaa hayo ni kuwa inaondosha pengo kati ya tajiri na masikini na jengine kila mmoja katika jamii kufikia mahitajio yake ya msingi.

### 4. Saumu

Waislamu wanafunga kila mwaka katika Ramadhani, kuanzia alfajiri mpaka juna linapozama. Wakati huo wanajiepusha na kula, kunywa na jimaa.

Saumu inaisafisha roho, huilea roho kusubiri na kuvumilia. Vilevile inatoa faida nyingi za kiafya.





## 5. Haji

Kwenda kuhiji katika Nyumba ya Allah Makkah ni jambo limefaradhishwa kwa kila muislamu angalau mara moja katika maisha.

Haji inapatikana mwezi wa 12 katika kalenda ya Kiislamu, ni nguzo ambayo kwayo kunaonekana umoja wa waislamu pasi na kujali rangi zao, ngozi zao, hadhi zao na miaka yao, wote wanashirikiana kumuabudu Allah. Safari hii kubwa ina vipengee vingi vya ibadah, kama kuchinja, safari na kusali sehemu tofauti. Uzoefu huu unamfanya mtu kuwa na unyenyenyeuku, subira na upole.

*Wenye kuhiji wote wanavaa mavazi ya kufanana na ya sawa, ambayo hayatofautishi kati ya tajiri, fakiri, mwenye nguvu, mnyonge, mfanya kazi na bosi wa kazi - wote wanakuwa sawa kwa kule kusimama kwao mbele ya Allah.*

# UELEWA WA 'IBADAH

## Ni kila kile anachokipenda Allah na kukiridhia.

Uelewa wa ibada katika uislamu hauishilii tu katika zile nguzo za Uislamu tano. Uelewa wa 'ibadah umekufanya vitendo vyote anavyovipenda Allah na kuviridhia. Matendo ya kila siku ya kawaida yanaweza kuwa ni ibadah ikiwa mtu atamtakasia nia yake Allah kwa sura ile Anayoitaka. Mfano wa hayo kunaingia kutabasamu, kumtendea wema jirani, kusaidia familia, kuwa mwaminifu na hata kuondosha chenye kuudhi njiani.

Inatakiwa itambulikane kuwa Allah hana haja ya ibadah ya yeyote. Kinyume chake mja ndiye aliye na haja ya kumuabudu Allah kwa manufaa yake.

## Hitimisho

Nguzo za Uislamu na za imani zilizotajwa ndizo zinazosimamisha kiini cha Uislamu.

Kuzitendea kazi nguzo za imani na Uislamu zilizotangulia kunamtimizia mtu haja zake za kiroho, za kimwili, za kinafsi na za kijamii katika maisha ya watu wote. Ni njia ya maisha kiutendaji kazi na kiakili. Jengine ni kuwa, ni njia ya pekee ya maisha anayoikubali Allah na kuiridhia. Vilevile ndio njia ya kipekee ambayo hatimae inayomfikisha mtu peponi.

*“Mwenye kutenda mema miongoni mwa wanamume au wanawake naye akiwa muumini, Tutamhuisha uhai mzuri na Tutawalipa malipo yao kwa mazuri zaidi ya yale waliyokuwa wakitenda.”*

Qur'aan 16:97








**HOTLINE**  
 +971 56 204 2045  
 islamicicdx

www.islamicic.com @info@islamicic.com +971 4 355 5223

SCAN QR CODE FOR E-VERSION OF FLYER

icdx.com/swahili

CONTENTS



سبيلك للسلام  
Your Path To Peace..  
**FREE COPY**



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

# MTUME MUHAMMAD (AMANI YA ALLAH IWE JUU YAKE)

SWAHILI [02/10]

النبي محمد عليه الصلاة والسلام

**NI LAZIMA UMŴUE MTU HUYU!**

PART OF




icelibrary.com | islamic.com



دائرة الشؤون الإسلامية والعمل الخيري | Islamic Affairs & Charitable Activities Department (2017/139)

# NI NANI MUHAMMAD? (AMANI YA ALLAH IWE JUU YAKE)

Waislamu wanaamini kwamba, mtume Muhammad (amani ya Allah iwe juu yake) ni mtume wa mwisho katika mtiririko mrefu wa mitume waliopelekwa kulingania watu katika kumtii na kumuabudu Allah pekee. Baadhi ya mitume hii ni Adam, Nuhu, Ibrahim, Ismail, Is-haq, Yakoub, Yussuf, Daud, Suleiman, na Issa (Yesu) rehema za Allah ziwe juu yao wote.




Na kama ambavyo Mussa (amani ya Allah iwe juu yake) aliteremshiwa Taurati, (wahyi wa asili ambao uliteremshwa kwa Mussa), na Issa nae aliteremshiwa Injili, (wahyi wa asili- sio toleo la sasa), waislam wanaamini kwamba mtume Muhammad nae ameteremshiwa Qur-an ili awabainishie watu yale waliyoteremshiwa na ili wawe wachamungu.








Na aliulizwa mama wa waumini, bi Aisha radhi za Allah ziwe juu yake, kuhusu wasifu wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na akajibu "Alikuwa ni Quran inayotembea juu ya ardhi yaani kwa hakika alikuwa akiyavaa mafundisho ya Quran katika maisha yake ya kila siku, na huenda tukaeleza vipi alikuwa mtume akifasiri mafundisho ya Quran tukufu katika matendo matukufu







# MTUME WA REHMA

Kwa hakika mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa halinganii watu kuhusu kusali, kufunga na kutoa zakka pekee, lakini alikuwa akiwafunza kwamba imani ya mtu kwa Allah ni lazima ifute upotevu na iathiri maingiliano yake na wengine, Amesema mtume "Mbora wenu ni yule mwenye tabia nzuri zaidi miongoni mwenu"



Na kwa hakika yameenea maneno ya Mtume (s.a.w) yanayohusisha uhusiano baina ya imani na matendo kwa mfano "mwenye kumuamini Allah na siku ya mwisho basi na asimuudhi jirani yake, na mwenye kumuamini Allah na siku ya mwisho na amkirimu jirani yake, na mwenye kumuamini Allah na siku ya mwisho basi na aseme kheri au anyamaze" Bukhari (6018)





Na amefundisha mtume wa mwisho matendo ya kibinaadamu kuhurumiana, na kuheshimiana, amesema mtume “asiemuhurumia mwenzake nae hatohurumiwa” Bukhari (5997)

Na imepokewa kwamba baadhi ya masahaba walimtaka mtume amuombe Mungu aongeze adhabu yake kwa washirikina lakini alijibu, “sikuteremshwa kama mwenye kulaani, bali mimi nimeteremshwa niwe rehema (kwa viumbe wote).” Muslim (2599)

## MSAMAHA

Alikuwa mtume (s.a.w) ni mwingi wa msamaha, na mwenye moyo mzuri mno, anapomuudhi mtu yeye humsamehe, na kila yalipozidi maudhi ya mtu kwake, yeye huzidisha subira. Na alikuwa mwingi zaidi wa usamehevu, hasa hasa pale anapokuwa na amri, na nguvu kulipiza alilotendewa.

Amesema Allah mtukufu, “na wasamehe na waachilie mbali (wapuuze yaliopita), jee nyinyi hampendi Allah akusameheni?”

An-Nuur 22

Alikuwa mtume (amani ya Allah iwe juu yake) ni mwenye kudumu kuomba msamaha wala hakukuwa na kosa kubwa lisiloweza kusamehewa na yeye na alikuwa ni kigezo chema katika kusamehe, na kuomba msamaha, na uvumilivu na kusahau, kama alivotolewa mfano kwa kauli ya Allah.

“Shikamana na kusamehe na amrisha mema na wapuuze wajinga”

Al-A'raf 199

## USAWA

Katika hadithi zifuatazo anafundisha mtume (amani ya Allah iwe juu yake) kwamba binaadamu wote ni sawa mbele ya Allah.

“kwa hakika mboru wenu mbele ya Allah ni yule mchamungu zaidi miongoni mwenu”

Al-Hujuraat 13

Amesema mtume (amani ya Allah iwe juu yake) “kwa hakika baba yenu ni Adam, na Adam anatokana na udongo, hakuna ubora kwa muarabu dhidi ya asiekuwa mwarabu, wala mweusi dhidi ya mwekundu, isipokuwa kwa uchamungu” Ahmad (23489)

Vile vile amesema mtume (amani ya Allah iwe juu yake) “hakika Allah mtukufu haangalii sura zenu, wala mali zenu, lakini anaangalia katika nyoyo zenu na matendo yenu” Muslim (2564)

Na imepokelewa kwa mmoja wa masahaba wa mtume (amani ya Allah iwe juu yake) alimwita sahaba mwengine vibaya, “ewe mtoto wa mwanamke mweusi!” akakasirika mtume kwa jambo hilo na akasema “unamuabisha kwa weusi wa mama yake? Kwa hakika bado una chembe za ujinga” Bukhari (30)

# UVUMILIVU

Na imepokewa kuhusu wasifu wa mtume wa mwisho kwamba “alikuwa halipi uovu kwa uovu lakini husamehe na huwachilia mbali” Bukhari (4838)

Na kama hivi ndivyo alivyokuwa akifanya mtume pale aliponyimwa haki yake, na kufanyiwa uadui kwa nafsi yake.

Misingi ya uislamu imekusanya matukio mengi kuhusu sehemu ambazo mtume angeliweza kulipiza (kisasi) kwa aliemuudhi na kumfanyia ubaya, lakini yeye alisamehe.

Na alikuwa akiwafundisha watu kuwa na subira katika shida na majanga, amesema mtume (amani ya Allah iwe juu yake) “si mwenye nguvu ambae anapigana mieleka bali mwenye nguvu ni yule anaeziua nafsi yake wakati wa kukasirika kwake” Bukhari (6114)

Kufanya subira na uvumilivu, haina maana kwamba lazima muislamu awe anakubali kila kitu na asijilinde anaposhambuliwa. Anasema Mtume (amani ya Allah iwe juu yake) “musitamani kukutana na adui, na muombeni Allah msamaha na mkukikutana nao basi fanyeni subira” Bukhari (2966)

“Mambo mazuri na mabaya hayawi sawa ondosha (ubaya unaofanyiwa kwa wema) tahamaki Yule ambae baina yako na yake kuna uadui atakuwa kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia uchungu”  
Fuswilat 34

# UPOLE






Na alisema mmoja wa masahaba ambaos walimuhudumikia mtume (amani ya Allah iwe juu yake) kwa miaka 10 kwamba alikuwa mpole kwake na akasema “hakuwahi kunambia kwa jambo lolote n lilolifanya “kwanini umefanya hivi?” na wala hakusema kwa jambo ambalo sikulifanya, “kwanini hukufanya hivi?” Ahmad (12784) na alikuwa ni mwingi wa mapenzi (ya kuwapenda wengine)” Ahmad (12784).

Na (mtume) aliwahi kumrudi mmoja katika wakeze pale alipokasirika alipotukanwa na mmoja katika watu.

Alimnasihi mtume (amani ya Allah iwe juu yake) akisema “poa ewe Aisha, hakika Allah ni mpole anapenda upole katika mambo yote” Bukhari (6024)

Na amesema vile vile “haukuwa upole katika jambo isipokuwa hulipamba, na wala haukuondoshwa katika jambo isipokuwa huliharibu” Muslim (2594)

“Basi kwasababu ya rehema itokayo kwa Allah umekuwa laini kwao, na kama ungelikuwa mkali na mwenye moyo mgumu bila ya shaka wangelikukimbia”  
Aali-Imran 159



# UNYENYEKEVU

Alikuwa mtume (amani ya Allah iwe juu yake) akiwazuia watu kusimama kwa heshima yake, na akikaa sehemu yoyote, na hakuwa akivaa nguo zinazomtofautisha na masahaba zake (radhi za Allah ziwe juu yao) na amezoea kuchanganyika na mafakiri na maskini, na kukaa na wazee, na kusaidia wajane, na wala haikuwezekana kwa wasiomjua kumtofautisha awapo katikati ya watu.

“Na waja wa Allah(anaowapenda ni wenye sifa hizi) ni wenye kwenda ulimwenguni kwa unyenyekevu na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu (maneno ya) salama”

Al-Furqan 63

Na aliwahunubia masahaba zake akisema “kwa hakika Allah amenifunulia kwamba munyenyekee, na asijifakharishe mmoja kwa mwenzake, na mtu yoyote asimnyanyase mwenzake” Muslim (2865)

Na katika yanayojuulisha unyenyekevu wake ni kuogopa kumuabudu asiekuwa Allah, amesema mtume (amani ya Allah iwe juu yake)

“Musichupe mpaka katika kunisifu kama walivyochupa mipaka manasra katika kumsifu Issa bin Maryam kwa hakika mimi ni mja , basi semeni mja wa Allah na mtume wake” bukhari (3445)







# MUME WA MFANO

Amesema mama wa waumini, bibi Aisha (Allah amuwie radhi) “alikuwa mtume wa Allah (amani ya Allah iwe juu yake) akihudumia watu wake, akishona nguo zake, na akitengeneza viatu vyake, na akifanya kazi za nyumbani kwake kama anavyofanya mmoja wenu nyumbani kwake” Ahmad (25341)

“na kaeni nao kwa wema”

An-Nisai 19


Na hakuwa mtume (amani ya Allah iwe juu yake) ni mwema kwa watu wa nyumbani kwake pekee, kwa hakika aliwasisitiza masahaba zake kufuata mfano wake, amesema mtume (amani ya Allah iwe juu yake) “Mkamilifu katika waumini kwa imani, ni yule mwenye tabia nzuri, na mpole wao kwa watu wake”



# KIGEZO CHEMA

Kilichotangulia ni kichache mno katika maisha ya mtume (amani ya Allah iwe juu yake).

Na katika mambo ya muhimu ni kwamba tulipotaka kujifunza uislamu tulikwenda moja kwa moja katika misingi ya asili, Quran, na maneno na vitendo vya mtume Muhammad (amani ya Allah iwe juu yake), na si uadilifu kwa mtu kuhukumu kitu kuhusu uislamu kwa makosa yanayofanywa na baadhi ya waislamu.









## VIPI WANASEMA ASIOKUWA WAISLAMU KUHUSU MTUME (amani ya Allah iwe juu yake)

Mahatma K Gandhi, kiongozi mkubwa wa kisiasa na kiongozi wa kiroho wa India anasema

*“Ulikuwa urahisi ulio mgumu kutomzingatia kabisa mtume Muhammad (amani ya Allah iwe juu yake), ukweli wake na kujali kutekeleza ahadi zake, na mapenzi yake ya dhati kwa masahaba zake, na ushujaa wake, na kumwamini na kumtegemea Mungu wake katika mambo yake. Mambo haya ndio yaliyofanikisha kila jambo na kuweza kuepuka vikwazo vyote na sio upanga (alioutumia).*

George Bernard Shaw amesema katika kitabu chake

*“Dunia zama hizi inahitaji mtu kama Muhammad, watu wa dini katika zama za kati, kwasababu ya ujinga na ugumu wao, walimfanya (Muhammad) kama mtu mbaya, walichukulia kama adui wa masihi, lakini baada ya kuangalia kwa kina hadithi ya mtu huyu nimemuona kama ni mtu mzuri sana na wa maajabu na nimefikia uamuzi kwamba hakuwa adui wa ukristo na ni lazima aitwe mwokozi wa watu. Kwa maoni yangu, angepewa mamlaka ya kuongoza dunia ya sasa angeliweza kutatua matatizo yetu, na kuhakikisha amani na furaha ambayo dunia hii inaitafuta”.*



HOTLINE

+971 56 204 2045










islamicicdx



www.islamicic.com @info@islamicic.com +971 4 355 5223

SCAN QR CODE FOR E-VERSION OF FLYER

icdx.com/swahili



سبيلك للسلام  
Your Path To Peace..  
**FREE COPY**



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

# MTUME WA ALLAH ISSA BIN MARYAM (YESU)

SWAHILI [03/10]

النبي عيسى عليه الصلاة والسلام

Waislamu Wanampenda  
Issa Bin Maryam (Yesu)  
Amani Ya Allah Iwe Juu Yake








PART OF



icelibrary.com | islamicic.com



دائرة الشؤون الإسلامية والعمل الخيري  
Islamic Affairs & Charitable Activities Department  
(2017/139) |



Yesu ni mtu anaependwa na mabilioni ya watu duniani, lakini bado kuna tofauti kuhusu mtu huyu. Waislamu na wakristo wote wanampenda na kumuheshimu Yesu lakini katika hali tofauti.

Makala hii inakusudia kuweka wazi baadhi ya kadhia zinazohusiana na masihi (Yesu), kama vile “Je! Yesu alikuwa Mungu au alipelekwa na Mungu? Yesu alikuwa nani?”

## “YESU KAMA MUNGU”

Wanazua baadhi ya wakristo kwamba Yesu ni Mungu au ni mmoja kati ya waungu watatu, na kwamba yeye ni mungu alieishi duniani katika umbile la mwanaadamu. Lakini Biblia imeleza kwamba Yesu alizaliwa, akala, akalala, akasali, na alikuwa na elimu yenye mipaka, mambo ambayo si sifa za Mungu. Mungu ana sifa ya Ukamilifu tofauti na mwanaadamu. Vipi inawezekana vitu viwili kuwa sawa na tofauti kwa wakati mmoja?

Uislam unafundisha kwamba Mungu siku zote ni mkamilifu. Kuamini Mungu alijifanya mwanaadamu ili aweze kudai kuwa yeye ni Mungu si ukamilifu. Mkristo yoyote lazima ajiulize, hii fikra ya Mungu ambae mwanzo alikuwa mtoto dhaifu, asieweza kumsaidia yeyote, aliekuwa hawezi kuishi bila ya kula, kunywa na kulala, ndie huyo huyo Mungu mtukufu aliyeelezewa katika Agano la kale? Bila ya shaka sie huyu.

Mtu anaweza kujiuliza “kama Mungu anaweza kufanya lolote kwanini ashindwe kujifanya kama mtu?” Katika maana za Mungu ni kwamba Mungu hawezi kufanya mambo ya kibinaadamu, Mungu hafanyi mambo ambayo yatamfanya awe kama si Mungu. Kama Mungu angelijifanya kama mtu na akafanya matendo ya watu basi asingelikuwa Mungu tena.






Baadhi ya aya za biblia zenye utata zinaweza kuonesha kuwa Yesu alikuwa kiumbe wa ajabu. Lakini tukiangalia aya nyengine zinaonesha kuwa Yesu ni mtu tofauti na watu wengine lakini si zaidi ya hivyo. Biblia ina aya nyingi ambazo Yesu anazungumza na kuonesha (kimatendo) kama yeye na Mungu ni tofauti. Kwa mfano:

Yesu: akaanguka kifulifuli akaomba” (Mathayo 26:39). Sasa kama yesu angelikuwa Mungu, je! Angelianguka kifulifuli na kuomba? Na angelikuwa anamuomba nani?

Biblia imemuita Yesu kuwa ni Nabii (Mathayo 21: 10-11), kwahivyo Yesu atakuwaje Mungu na awe nabii wa Mungu kwa wakati mmoja?

Yesu alisema “nakwenda kwa baba, kwa maana baba ni mkuu kuliko mimi” Yohana 14:28

Yesu alisema “ninapaa kwenda kwa baba yangu naye ni baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu” Yohana 20:17



kama Yesu angelikuwa Mungu, kwanini aseme “ kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu”? na alikuwa anapaa kuelekea wapi?

Kama Yesu angelikuwa Mungu bila ya shaka angeliwaambia watu wamuabudu na kungelikuwa na aya za biblia ambazo zingetaja mambo haya, lakini yeye amefanya kinyume chake na amekataza kuabudiwa yeye na akasema “ nao waniabudu bure” Mathayo 15:9

## “MTOTO WA MUNGU”

Wanazua baadhi ya wakristo kuwa Yesu ni mwana wa Mungu. Hii inamaanisha nini? Mungu ametakasika kuwa na mtoto wa kimaumbile. Binaadamu wana watoto ambao ni wanaadamu vile vile, paka nao wana watoto ambao ni paka, inamaanisha nini kuwa Mungu ana mtoto?








“ Haiwi kwa Allah kufanya mtoto, Ametakasika. Anapotaka jambo basi huliambia tu kuwa nalo likawa”  
(Maryam 35)

Ukiwacha tafsiri ya neno kwa neno, maana ya “mwana wa Mungu” kama ilivyotumika na lugha ya biblia ni “mtu mwema” na limetumika neno hili kwa mtume Daud, na Suleiman, na Yaqoub – halikutumika kwa Yesu pekee “Israeli ni mwanangu mimi, mzaliwa wa kwanza wangu” (Kutoka 4:12). Kiukweli, kwa lugha ya biblia mtu yoyote aliyekuwa mwema huitwa mwana wa Mungu “kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu hao ni wana wa Mungu” [Waroma 8:14]

## “BABA NA MOLA MLEZI”

Vile vile, hili neno Baba likitumika kuashiria Mungu halitakiwi kuchukuliwa kwa maana halisi ya baba, badala yake ni njia ya kusema kwamba Mungu ndio muumba, msaidizi na bwana wa viumbe wote. Kuna aya nyingi zitakazotusaidia kujua maana ya neno “Baba” kwa mfano “Mungu mmoja naye ni Baba wa wote” [Waefeso 4:6]

Vile vile baadhi ya nyakati Yesu aliitwa “bwana” na wanafunzi wake. Neno hili linatumika katika lugha ya asili ya biblia, kwa kuashiria Mungu au watu wa tabaka la juu. Kwa mfano katika agano la kale la Ugiriki neno kyriosis limetumika kuashiria bwana na jina la mmiliki wa shamba la zabibu vile vile Mathayo 20:8, na bwana aliempiga mtumishi wake asiemtii (Luka 20.42-47)



Na katika sehemu nyengine za biblia, Yesu ameitwa mtumishi wa Mungu na wanafunzi wake “Mungu wa baba zetu, amemtukukuza mtumishi wake Yesu” [Matendo 3:13]. Hii inaonesha wazi wazi kwamba neno bwana likitumika kwa Yesu, basi huwa ni kwasababu ya kumpa cheo na heshima na sio kwa maana kuwa yeye ni Mungu.

## YESU KAMA MTUME

Mayahudi wanakataa kwamba Yesu ndie masihi. Hii ni tofauti sana na ukristo ambako Yesu anaabudiwa kama mwana wa Mungu. Uislam upo katikati na unamtambua na kumzingatia Yesu kama ni Mtume na Mjumbe wa Allah na kwamba Yesu ndie Masihi lakini waislamu hawamuabudu yeye (Yesu) kwasababu Kuabudiwa anaabudiwa Allah pekee ambae yeye ndie aliemuumba Yesu na viumbe wote ulimwenguni.

“Haiwi kwa Allah kufanya mtoto, Ametakasika. Anapotaka jambo basi huliambia tu kuwa nalo likawa”

(Maryam 35)

## KUZALIWA KWA MIUJIZA

Kulingana na Qur-an malaika Jibril alitumwa kwa Sayyida Maryam (bikira Maria) katika umbile la mwanaadamu, ili akampe habari kuhusu kujifungua mtoto ambae atamzaa kimiujiza bila ya kuingiliwa na mwanamme.

“(Malaika) Akasema “hakika mimi ni mjumbe wa Mola wako, ili nikupe mwana mtakatifu”\* akasema niwezeje kupata mtoto hali hajanigusa mwanamume(yoyote kwa a ya halali) wala mimi si mwanamke mwenye kuzini?”\* (malaika)akasema ni kama hivyo (unavyosema , lakini) mola wako amesema haya ni sahali kwangu, na ili tumfanye muujiza kwa wanaadamu na rehema itokayo kwetu, na hili ni jambo lililokwisha kuhukumiwa” (Maryam 19-21)

Na wanadai baadhi ya watu kwamba kuzaliwa kwake (Yesu) kwa miujiza ndio ushahidi wa uungu wake. Lakini Yesu si wa mwanzo kutokuwa na baba, Nabii Adam(amani ya Allah iwe juu yake) yeye hakuwa na baba wala mama. Allah anasema: “Bila ya shaka hali ya Issa kwa Allah ni kama hali ya Adam, alimuumba kwa udongo kisha akasema “kuwa” na akawa\* (Hii) ni haki inayotoka kwa mola wako, basi usiwe mingoni mwa wanaofanya shaka” Aali- Imran 59-60

Kama Yesu anaabudiwa kwasababu hana baba, basi kwa hakika Adam ana haki zaidi ya kuabudiwa kwasababu yeye hana baba wala mama.

# MIUJIZA YA YESU

Yesu alizaliwa bila ya baba na alifanya miujiza mengi, kwa idhini na uwezo wa Allah.

Alizungumza utotoni katika mbeleko ili kumtetea mama yake dhidi ya shutuma za watu kwamba amezini. Qur-an inaeleza kuwa Yesu alihuisha wafu na aliponesha wenye ukoma na vipofu kwa idhini na uwezo wa Allah.

Ukweli kwamba Yesu alitenda miujiza haumanishi lolote zaidi ya kuwa yeye alikuwa mtumishi mwenye kunyenyekea kwa Allah. Kiukweli, mitume wote walitenda miujiza akiwemo, nabii Nuhu, na Mussa na Muhammad (amani ya Allah iwe juu yao) ambayo miujiza hii ilitendeka kwa uwezo na idhini ya Allah, ili kuthibitisha utume wao.

# UJUMBE WA YESU

Mitume waliotajwa katika Agano la Kale kama Ibrahimu, Nuhu na Yunus hawakuwahi kumlingania Mungu kwa dhana ya utatu na hawakuamini kwamba Yesu ndio mtetezi wao

Ujumbe wao ulikuwa mwepesi sana








(kufahamika): kwamba hakuna mola isipokuwa Allah na yeye ndie anaestahiki kuabudiwa". Haiingii akilini kwamba Mungu apeleke mitume kwa watu kwa miaka mingi halafu ghafla tu abadilishe utaratibu na atangaze kwamba yeye ni mmoja wa waungu watatu na atake tuamini kwamba Yesu ni Mungu.






*"Na alipofika Issa kwa dalili zilizowazi alisema "kwa hakika Allah ndiye mola wangu na mola wenu basi muabuduni hii ndio njia iliyonyooka"*

**(Qur-an 43: 63-64)**

Ukweli ni kwamba Yesu alilingania ujumbe walioulingania mitume wote waliopita kabla yake. Kuna ibara katika biblia inayoelezea ujumbe huu. Mtu mmoja alikuja kwa Yesu akamuuliza "katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza? Yesu akamjibu "ya kwanza ndio hii, sikia Israeli "bwana Mungu wetu ni Mungu mmoja tu" [Marko 12:28-29] kwahivyo amri kuu na imani ya muhimu zaidi kwa mujibu wa Yesu ni kwamba Mungu ni mmoja tu. Kama Yesu angelikuwa Mungu angelisema "Mimi ni Mungu, hivyo niabuduni" badala yake kutoka katika Agano la Kale (mara nyingi) alikuwa akirejea sentensi akithibitisha kuwa Mungu ni mmoja tu.

Jambo hili linaenda sambamba na kazi ya Yesu kama inavyoelezwa na Uislam kwamba Yesu alipelekwa kwa wana wa Israeli ili kuthibitisha ujumbe wa mitume iliopita kwamba wamuamini Mungu mmoja.





Na alikuwa (Yesu) amejisalimisha kwa Allah, mnyenyekevu na anaetekeleza amri za Allah kwahivyo alikuwa ni muislamu – kwa maana mtu yeyote anaetekeleza matakwa na amri za Allah (huitwa muislam).

## YESU KATIKA UISLAM

Yesu alikuwa mtume mtukufu alieletwa na Allah ili awalinganie watu kumwabudu Mungu mmoja pekee.

Na jambo hili liko wazi katika biblia na limethibitishwa katika Qur-an.


Imani ya Uislam kuhusu Yesu inaeleza vipi Yesu wa kweli alikuwa, sambamba na kulinda imani ya kweli kuhusu Mungu, ukubwa, upekee na ukamilifu wake.

Tunakuomba ujifunze zaidi na uchunguze Uislam. Na (huu) Uislamu si dini nyengine (mpya). Ni dini yenye ujumbe ule ule aliolingania Nuhu na Ibrahim na Mussa na Issa (Yesu) na Muhammad (amani ya Allah iwe juu yao). Uislam una maana ya “kujisalimisha kwa Allah” na ni mfumo wa maisha uliotimia ambao unahamasisha mtu kuchunga mahusiano yake na Mungu ambae ndio muumba wake. Uislam unafundisha kwamba Mungu ni muadilifu na mwingi wa rehema na habitaji kujitoa nafsi yake ili asamehe makosa ya watu, na wala hakuna mtu yoyote aliezaliwa na dhambi, Mungu anahukumu watu kwa makosa waliyoyatenda wao wenyewe, na kila mtu atawajibika kwa matendo yake mwenyewe.







Uislam unatufunza kuwapenda na kuwaheshimu mitume wote lakini mapenzi yetu na heshima yetu kwao isiwe na maana ya kwamba tuwaabudu, kwani haabudiwi isipokuwa Allah pekee. Kumtambua Yesu kama mtume wa Allah na kuwa muislam hakuna maana kwamba unabadilisha dini yako, bali huko ndio kufuata maamrishi ya asili ya

**HOTLINE**  
 +971 56 204 2045  
 islamicicdxb

islamicic.com @ info@islamicic.com +971 4 355 5223



CONTENTS



سبيلك للسلام  
Your Path To Peace..

**FREE COPY**


مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

# WAZO WA MUNGU katika UISLAMU

SWAHILI [04/10]      مفهوم الإله في الإسلام


*Hakuna Mkwabwa  
Zaidi ya Muumba*

PART OF




المكتبة الإلكترونية الإسلامية  
**ISLAMIC**  
e-LIBRARY

[icelibrary.com](http://icelibrary.com) | [islamicic.com](http://islamicic.com)



www.daralber.ae



الإمارات  
THE EMIRATES

دائرة الشؤون الإسلامية والعمل الخيري | Islamic Affairs & Charitable Activities Department  
(2017/139) | تمديد رقم

# Je, Kuna Mungu?

Kuna sababu nyingi za kimantiki za kuamini kuwepo kwa Mungu. Sababu tatu rahisi zinaelezwa hapa chini:

## 1. Mpangilio wa Ulimwengu

Fikiria unatembea ufukweni na unakuta saa kwenye mchanga. Je, unaweza kuamini kwamba saa hiyo ilijitokeza yenyewe? Hutaamini kwamba saa hiyo ilitokea tu kwa bahati nasibu kutoka kwenye mchanga. Sehemu zake zote tata haziwezi tu kuibuka kutoka kwenye vifaa vilivyokuwa vimezikwa ardhini. Saa lazima iwe na mtengenezaji. Na kama saa hiyo inaonyesha muda sahihi, tunatarajia mtengenezaji wake lazima awe na akili. Matukio ya kiasili hayawezi kutoa saa inayofanya kazi.

Fikiria sayari ya dunia. Mzunguko wake unadhibitiwa kwa usahihi sana kuizunguka jua kiasi kwamba wanasayansi wanaweza kuchapisha kwa usahihi nyakati za kuchomoza na kuchwa kwa jua mapema. Kama vile saa ilivyo na mtengenezaji mwenye akili kudumisha muda sahihi, basi dunia pia lazima iwe na Muumba Mwenye akili kudumisha muda sahihi wa kuzunguka jua. Je, hili lingeweza kutokea lenyewe?!

Vivyo hivyo, tunapona mpangilio, sheria sahihi na mifumo ndani yetu na katika ulimwengu mzima, si ni kimantiki kuamini kwamba ulimwengu una Mpangiliaji? Mpangiliaji Huyu Anaelezwa vyema zaidi kama Mungu – Yule Aliyesababisha mpangilio katika ulimwengu.

## 2. Mwanzo wa Ulimwengu




Sayansi ya kisasa inakubali kwamba ulimwengu una mwanzo. Hii inatokana na ugunduzi wa hivi karibuni kuwa ulimwengu unapanuka, na tukirudi nyuma kwa wakati, ulimwengu unakutanika – hali inayodhihirisha mwanzo wake. Kuna maelezo matatu yanayowezekana kwa mwanzo wa ulimwengu. Aidha:






1. Ulimwengu ulitokea kutoka pasina kitu,
2. Ulimwengu ulijiumba yenyewe, au
3. Ulimwengu uliumbwa.

Kuhusu maelezo ya pili, mantiki rahisi inatufundisha kwamba kitu hakiwezi kufanya chochote kabla ya kuwepo. Hivyo, maelezo ya tatu ndilo penye mantiki: kiumbe chenye nguvu na akili, yaani Mungu, ndicho kilichoumba ulimwengu.

*Uzoefu wa kibinadamu unaonyesha kwamba kitu chenye mwanzo hakiwezi kutokea tu kutoka pasina kitu.*

Watu wengine wanaweza kuuliza, “Nani alimwumba Mungu?”





Mungu, Muumba, ni tofauti na uumbaji wake. Kama angekuwa sawa na uumbaji wake, naye pia angehitaji muumba, jambo linalosababisha mfululizo usio na mwisho wa waumba, jambo ambalo haliwezekani. Yeye yupo nje ya wakati na mambo ya kimwili ya ulimwengu huu. Mungu amekuwepo daima na hana mwanzo; kwa hiyo swali la nani alimwumba Mungu halina mantiki.

### 3. Ufunuo kutoka kwa Mungu

*Kama Mungu aliteremsha kitabu cha mwongozo kwa wanadamu, tungetarajia kitabu hicho kiwe na ushahidi wazi wa kuwepo kwa Mungu.*

Kuna dalili wazi kwamba kitabu cha Uislamu, Qur'an, ni neno la Mungu. Hapa chini kuna muhtasari mfupi wa sababu zinazounga mkono dai hili:

- Qur'an iliteremshwa zaidi ya miaka 1400 iliyopita na ina ukweli mwingi wa kisayansi ambao haukujulikana kwa watu wa wakati huo na ambao umethibitishwa hivi karibuni na sayansi ya kisasa.

Mifano ni kama vile:

- "Maji kuwa chanzo cha uhai" (Qur'an 21:30);
- "Upanuzi wa ulimwengu" (Qur'an 51:47);
- "Na mizunguko ya jua na mwezi" (Qur'an 21:33).

- Qur'an ina ukweli mwingi wa kihistoria ambao haukujulikana kwa watu wa wakati huo pamoja na unabii mwingi ambao umethibitishwa kuwa kweli.
- Qur'an haina makosa wala migongano.
- Qur'an imehifadhiwa, neno kwa neno, tangu ilipoteremshwa kwa lugha yake asilia ya Kiarabu, tofauti na maandiko mengine ambayo hayapo tena kwa umbo lake asilia.
- Ujumbe wa Qur'an ni rahisi, safi na wa ulimwengu mzima unaovutia imani za asili za mwanadamu kuhusu Mwenyezi Mungu.
- Qur'an iliteremshwa kwa Mtume Muhammad (amani iwe juu yake) ambaye anajulikana kihistoria kuwa hakuwa na elimu ya kusoma na kuandika. Hata hivyo, Qur'an ina mtindo wa kipekee wa lugha unaojulikana kote kama kilele cha ufasaha na uzuri wa lugha ya Kiarabu.

*Ufasiri wa kimantiki zaidi kwa vipengele vya kipekee na umuujiza wa Qur'an ni kwamba imetoka kwa Mwenyezi Mungu.*

# Mungu ni Nani?

“Allah” ni jina maalum la Mungu Mmoja wa Kweli. Hakuna kitu kingine kinachoweza kuitwa Allah. Jina hili halina wingi wala jinsia tofauti na neno la Kiingereza “God” ambalo linaweza kuwa wingi na la kike (mfano: gods/goddess). Matumizi ya kipekee ya “Allah” yanaonyesha msisitizo wa Uislamu juu ya usafi wa imani katika Mungu Mmoja.

*Na Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Hakuna mungu ila Yeye.”*  
 Qur'an 2:163

Uzuri mkuu wa Uislamu ni kwamba unakiri ukamilifu, uadhimu na upekee wa Mwenyezi Mungu pasina na pingamizi kamwe. Huu unaonyeshwa kwa mafundisho safi ya Uislamu kwa sifa za Mungu Mwenyezi.

## Mungu ni Mmoja na wa Kipekee:

- Mungu hana mshirika, hana sawa wala mpinzani.
- Mungu hana baba, mama, wana, mabinti wala wake.
- Ni Mungu peke yake anayestahili kuabudiwa kikamilifu.
- Kama kungelikuwa na miungu zaidi ya mmoja, ingedhihirisha upungufu katika uwezo au mamlaka ya Mungu kwa kuwa hili lingehusisha ushindani, maridhiano au haja ya makubaliano kati ya miungu.

## Mungu ni Mwenye Nguvu Zote:







- Mungu ana mamlaka kamili na uwezo juu ya kila kitu.
- Kila kitu kinamtegemea Yeye kikamilifu na kinamtii kwa ukamilifu.
- Kumtii Mungu hakumuongezei nguvu, wala kumuasi hakumpunguzii nguvu hata kidogo.





## Mungu ni wa Juu Zaidi:

- Hakuna kilicho juu au kinachoweza kulinganishwa na Mungu.
- Sifa za Mungu haziwezi kufanana na sifa za viumbe Wake.
- Hakuna sehemu yoyote ya Mungu iliyopo ndani ya mtu au kitu chochote.
- Mungu ni mkamilifu na hana upungufu wowote wa kibinadamu, kama kupumzika siku ya saba baada ya kuumba ulimwengu, kama inavyodaiwa na baadhi ya dini nyingine.

## Mungu ni Mwenye Haki Kamili na Mwenye Rehema:

- Mungu hahitaji kujitoa sadaka ili kusamehe dhambi, wala hakuna mtu aliyezaliwa katika dhambi.





- Mungu humhukumu kila mtu kwa matendo yake mwenyewe na kila mtu anawajibika kwa vitendo vyake binafsi.
- Binadamu wanaweza kupata radhi za Mungu kupitia imani, tabia njema na uchamungu – si kwa sababu ya kabila, mali au hadhi ya kijamii

# ASILI YA YESU (ISA)

Wakristo wengi hudai kuwa “Yesu ni Mungu” – yaani, ni Mungu aliyeshuka duniani na kuchukua umbo la kibinadamu.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Biblia, Yesu alizaliwa, alikula, alilala, aliomba na alikuwa na maarifa yaliyokuwa na mipaka – mambo yote haya hayafai kuwa ya Mungu. Mungu ana sifa za ukamilifu ilhali mwanadamu ni kinyume chake. Hivyo basi, ni vipi kitu kimoja kiwe vitu viwili vinavyopingana kwa wakati mmoja? Hili halina mantiki.

*Wakati wa kuelezea dhana ya Mungu katika Uislamu, ni muhimu kufafanua nafasi ya Yesu (Isa), kutokana na mkanganyiko mkubwa na madai kuhusu asili yake.*

Lakini wengine huuliza, “Kama Mungu anaweza kufanya chochote, kwa nini asijigeuze kuwa mwanadamu?” Kwa maana ya kweli, Mungu hafanyi matendo yasiyostahili Uungu Wake. Hivyo basi, kama Mungu angekuwa mwanadamu na kuchukua sifa za kibinadamu, basi kwa lazima, asingeweza tena kuwa Mungu.

Zaidi ya hayo, Biblia ina aya nyingi ambapo Yesu anazungumza na kutenda kana kwamba Mungu ni nafsi tofauti na yeye. Kwa mfano, Yesu alisema: “Lakini sasa mnataka kuniua, mimi mwanadamu niliyewaambia ukweli niliousikia kutoka kwa Mungu.” [Yohana 8:40].

Wakristo wengi pia hudai kuwa “Yesu ni Mwana wa Mungu” lakini tujiulize, hili linamaanisha nini hasa?

Kwa hakika, Mungu yuko mbali na kuwa na mwana kwa maana halisi na ya kimwili. Kwa kweli, tunakuta neno “Mwana wa Mungu” likitumika kwa maana ya mfano kwa watu wema katika lugha za kale za Biblia. Linatumika mara kwa mara katika Agano la Kale kwa watu wema wengi kama vile Daudi, Suleiman na Israeli – si kwa Yesu pekee.

*Haimfai Mwenyezi Mungu kuchukua mwana; Yeye ni mkamilifu na hana kasoro!”*  
Qur'an 19:35

Mfano mmoja ni: “Israeli ni mzaliwa wangu wa kwanza,” (Kutoka 4:22).

Imani ya Kiislamu kuhusu Yesu inaeleza Yesu halisi alikuwa nani, huku ikidumisha imani safi kuhusu Mungu na Utukufu Wake. Yesu alikuwa Mtume mwenye heshima aliyetumwa na Mungu kuwaongoza watu kumwabudu Mungu pekee

## Mungu Pekee Anastahili Kuabudiwa

“Na mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na kitu chochote.” **Qur'an 4:36**

Uislamu unafundisha kuwa sala na ibada zote zinapaswa kumuelekezwa Mungu pekee. Hakuna kitu kingine chenye kustahili kuabudiwa: si sanamu, makaburi, jua, mwezi, wanyama, Manabii, watakatifu, malaika, makuhani au wasomi wa dini. Vyote hivi ni viumbe vilivyo na mipaka, na hivyo havifai kuabudiwa, ilhali Mwenyezi Mungu ni mkamilifu.



## Mungu Anaabudiwa Moja kwa Moja

Mungu hahitaji washirika wala waombezi. Kila mtu anaweza kumwabudu Mungu moja kwa moja, kwani Yeye husikia wote wanaomsifu na kumwomba. Kumwabudu Mungu kupitia njia isiyo ya moja kwa moja (k.m. kupitia sanamu, vinyago au waombezi) huonekana kama kuharibu Upweke wa Mungu na usafi wa ibada ambayo ni haki Yake pekee.

## Manabii Wote Walilingania Ibada ya Mungu

“Na kwa kila taifa tuliwatumia Mtume (tukiwaambia): ‘Mwabuduni Mwenyezi Mungu na jiepusheni na miungu wa uongo.’” **Qur'an 16:36**

Waislamu wanawaamini Manabii wote waliotumwa na Mungu. Manabii hawa ni pamoja na Adamu, Nuhu, Ibrahimu, Musa, Yesu na Muhammad. Wote walikuja na ujumbe mmoja – kuwaita watu wao waamini na waabudu Mungu Mmoja wa Kweli.

## Kusudi la Maisha ni Kumwabudu Mungu

Kusudi kuu la maisha ni kutambua ukuu wa Mungu, kuanzisha uhusiano wa moja kwa moja Naye, na kumwabudu Yeye pekee. Dhana ya ibada katika Uislamu haijafungiwa tu kwenye ibada kama sala na kufunga, bali inajumuisha matendo yote yanayompendeza Mungu kama vile kuwa na tabia njema, kuwa mwaminifu, kusimamia haki, kuwa na subira na kuwasaidia wahitaji.

Hitimisho, msingi wa Uislamu ni imani katika Umoja na Upekee wa Mwenyezi Mungu, ambaye ni Muumba na Mola wa kila kitu, mkamilifu kwa sifa Zake zote. Yeye pekee ndiye anayestahili kuabudiwa. Ndani ya hili ndipo pana mafanikio yetu katika maisha haya na maisha yajayo.

**HOTLINE**





**+971 56 204 2045**

islamicic.com @ info@islamicic.com +971 4 355 5223

**islamicicdx**

SCAN QR CODE FOR E-VERSION OF FLYER iicdx.com/swahili

CONTENTS



سبيلك للسلام  
Your Path To Peace..  
**FREE COPY**



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

# QUR'AN

SWAHILI [05/10]

القرآن

*Ufunuo wa Mwisho  
kwa Wanadamu*

PART OF



icelibrary.com | islamicic.com



دائرة الشؤون الإسلامية والعمل الخيري  
Islamic Affairs & Charitable Activities Department

# QUR'AN NI NINI?

## NENO LA MUNGU

Qur'an ni neno halisi la Mungu, Mwenyezi Mungu (Allah kwa Kiarabu), lililoteremshwa kwa Mtume Muhammad (amani iwe juu yake) kupitia Malaika Jibril.

*“Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.”*

Qur'an 39:1

## MWONGOZO KWA WANADAMU

*Kwa kifupi, Qur'an ni “mwongozo kwa wanadamu... na ubainisho (wa baina ya haki na batili).”*

Qur'an 2:185

Inatoa mwelekeo wa kuwasaidia wanadamu kuhukumu baina ya haki na batili, pasipo hivyo, mwanadamu bila shaka atakuwa katika hasara.

## UFUNUO WA MWISHO

Qur'an ni kitabu cha mwisho kilichoteremshwa na Mwenyezi Mungu, kikithibitisha kile kidogo cha ukweli kilichosalia katika baadhi ya maandiko ya awali na kupinga pamoja na kusahihisha uongo na nyongeza zilizojipenyeza katika matoleo ya sasa ya maandiko hayo.

*“Enyi mliopewa Kitabu! Aminini yale tuliyoyateremsha yakithibitisha yale yaliyoko kwenu...”*

Qur'an 4:47








# QUR'AN

## ILITEREMSHWA VIPI?

Qur'an iliteremshwa kwa Muhammad (amani iwe juu yake) na ipo tu kwa lugha aliyoteremshiwa nayo - Kiarabu. Hata hivyo, tafsiri ya maana ya Qur'an inapatikana kwa lugha nyingi.

Qur'an haikuteremshwa kama kitabu kamili kwa wakati mmoja; bali ufunuo wake ulienea kwa kipindi cha miaka 23.

Kwa sababu hii, ni muhimu kufahamu mazingira ambayo aya ziliteremshwa ili kupata uelewa sahihi wa Qur'an; la sivo, mafundisho yake yanaweza kufasiriwa vibaya.



# Ninawezaje Kujua Kwamba Imetoka Kwa Mungu?

## HIFADHI

Qur'an ndicho kitabu pekee kitakatifu cha dini kilichokuwa kikisambazwa kwa muda mrefu, na bado kimebaki safi kama siku kilipoteremshwa. Hakuna kilichoongezwa, kuondolewa au kubadilishwa tangu kilipoteremshwa zaidi ya miaka 1400 iliyopita.

*“Hakika Sisi Tumeteremsha Ukumbusho, na hakika Sisi ndio tutakao ulinda.”*

**Qur'an 15:09**

Si kwamba Qur'an imehifadhiwa tu kwa maandishi, bali pia katika nyoyo za wanaume, wanawake na watoto. Leo hii, mamilioni ya watu wamehifadhi Qur'an yote kutoka mwanzo hadi mwisho.

## MIUJIZA YA KISAYANSI

Qur'an haipingani na sayansi ya kisasa bali huunga mkono ukweli wake. Moja ya mambo ya kushangaza kuhusu Qur'an ni kwamba ina aya nyingi zinazofanua kwa usahihi matukio ya kiasili katika nyanja mbalimbali kama vile embryolojia, hali ya hewa, astronomia, jiolojia na sayansi ya bahari. Wanasayansi wameona maelezo yake kuwa sahihi mno kwa kitabu cha karne ya 7.







*“Tutawaonyesha Ishara Zetu katika ulimwengu na katika nafsi zao, mpaka iwadhahirikie kwamba huu ni Ukweli.”*






**Qur'an 41:53**

Kwa hakika, miujiza mingi ya kisayansi iliyotajwa katika Qur'an imegunduliwa hivi karibuni tu, kupitia maendeleo ya kisasa ya vifaa vya kiteknolojia. Fikiria yafuatayo:

- Qur'an inatoa maelezo ya kina ya maendeleo ya kijusi cha binadamu. Maelezo haya hayakujulikana kwa jamii ya wanasayansi hadi nyakati za karibuni.
- Sayansi ya kisasa imegundua kuwepo kwa viziwi vinavyoruhusu bahari mbili kukutana lakini kila moja ikihifadhi joto, msongamano na chumvi yake.

Ishara hizi za Mungu zilielezwa waziwazi katika Qur'an zaidi ya miaka 1400 iliyopita.





## UPEKEE

Tangu ilipoteremshwa, hakuna mtu yeyote aliyewahi kuleta hata sura moja kama ya Qur'an kwa uzuri wake, ufasaha, utukufu, hekima, unabii, na sifa nyingine kamilifu.

*“Na ikiwa mna shaka juu ya yale tuliyomteremshia mja wetu, basi leteni sura moja mfano wake, na waiteni mashahidi wenu mbali na Mwenyezi Mungu ikiwa mnasema kweli.”*

**Qur'an 2:23**

Wale waliomkataa Mtume Muhammad (amani iwe juu yake) walishindwa changamoto hii, hata walipokuwa mahiri sana kwa lugha ya Qur'an. Changamoto hii bado haijajibiwa hadi leo.

## HAKUNA MIGONGANO

Wanadamu wanapoandika, lazima wakosee kama vile kosa la tahajia na sarufi, kauli zinazopingana, hitimisho lisiloeleweka, kupitiliza au kuacha taarifa, na makosa mengine.

*Lau ingekuwa ni kutoka kwa mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu, bila shaka wangekuta ndani yake khitilafu nyingi.”*

**Qur'an 4:82**

Qur'an haina migongano yoyote – iwe ni katika maelezo ya kisayansi ya mzunguko wa maji, embryolojia, jiolojia na uumbaji wa ulimwengu; ukweli wa kihistoria na matukio; au unabii.

## JE, MUHAMMAD HANGEWEZA KUIANDIKA?

Mtume Muhammad (amani iwe juu yake) alijulikana kihistoria kuwa hakujua kusoma wala kuandika. Hakuwa na elimu katika uwanja wowote ambao unaweza kueleza usahihi wa kisayansi na kihistoria, wala uzuri wa kifasihi wa Kitabu hiki cha ajabu. Uhakika wa maelezo ya kihistoria ya watu na jamii za zamani yaliyomo ndani ya Qur'an pia ni makubwa mno kuweza kuandikwa na mtu yeyote.

*“Na Qur'an hii si kwamba ingeweza kutungwa na asiyekuwa Mwenyezi Mungu.”*

**Qur'an 10:37**

# LENGO LA UFUNUO

## KUAMINI MUNGU MMOJA WA KWELI

*“Na Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Hapana mungu ila Yeye, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.”*

*Qur'an 2:163*

Jambo muhimu zaidi linalotajwa katika Qur'an ni imani kwa Mungu Mmoja wa Kweli. Mungu anatarifu kwamba hana mshirika, hana mwana, hana anayemfanana naye, na kwamba hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Yeye peke yake. Hakuna kitu chochote kinachofanana na Mungu na hakuna kiumbe chake anayemfanana naye. Qur'an pia inakanusha wazo la kumpa Mungu sifa na mipaka ya kibinadamu.

## KUKATAA MIUNGU WOTE WA UONGO

*“Na mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote.”*

*Qur'an 4:36*

Kwa kuwa Allah Peke Yake Ndiye Anayestahiki kuabudiwa, miungu wa uongo na wa kubuniwa ni lazima wakataliwe. Qur'an pia inakanusha wazo la kumhusisha mtu au kitu kingine na sifa za uungu.

Kusimulia Hadithi za Zamani

Qur'an ina masimulizi mengi yenye mafundisho yenye manufaa, ikiwa ni pamoja na hadithi za kweli za Manabii wa zamani kama vile, Adam, Nuhu, Ibrahim, Isa na Musa. Kuhusu hadithi hizi, Mwenyezi Mungu anasema:

*“Hakika katika hadithi zao kuna mawaidha kwa wenye akili.”*

*Qur'an 12:111*

## KUTUKUMBUSHA SIKU YA KIYAMA







Kitabu hiki Kitukufu kinatukumbusha kwamba kila mmoja ataonja mauti na atahukumikiwa kwa kila tendo na kauli yake:







*“Na tutasimamisha mizani za haki kwa Siku ya Kiyama, basi haitadhulumiwa nafsi yoyote hata chembe...”*

*Qur'an 21:47*

## KUTIMIZA NJIA SAHIHI YA MAISHA

Muhimu zaidi, Qur'an inafundisha kwamba lengo la maisha ni kumuabudu Mungu pekee, na kuishi maisha kulingana na njia Aliyoagiza. Katika Uislamu, ibada ni neno pana linalojumuisha vitendo na kauli zote (iwe hadharani au faraghani) ambazo Allah Anazipenda na Kuridhika nazo. Hivyo basi, kwa kufanya yale Anayoyaamrisha Allah, Muislamu anamuabudu Mungu na kutimiza kusudi lake la maisha. Mifano ya ibada kutoka Qur'an ni kama ifuatavyo:





**Kuswali:** “Enyi mlioamini! Pigeni magoti na msujudu, na muabuduni Mola wenu, ili mpate kufanikiwa.” Qur’an 22:77

**Kutoa sadaka:** “...Na toeni, ni bora kwa nafsi zenu; na anayejiepusha na tamaa ya nafsi yake, hao ndio waliofanikiwa.” Qur’an 64:16

**Kuwa mkweli:** “Wala msichanganye haki na batili, wala msifiche haki hali mnajua.” Qur’an 2:42

**Kuwa na haya:** “Waambie Waumini wanaume wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao. Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao.” Qur’an 24:30-31

**Kuwa mwenye shukrani:** “Na Mwenyezi Mungu Amekutoeni matumboni mwa mama zenu – hamkujua chochote – na Akakupeni kusikia na kuona na nyoyo ili mpate kushukuru.” Qur’an 16:78

**Kuwa mwadilifu:** “Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi wa uadilifu, mashahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapokuwa ni dhidi ya nafsi zenu, au wazazi wenu, au jamaa zenu, na ikiwa ni tajiri au masikini, Mwenyezi Mungu anastahiki zaidi...” Qur’an 4:135

**Kuwa na subira:** “Na uwe na subira. Hakika Mwenyezi Mungu Hapotezi malipo ya wanaofanya mema.” Qur’an 11:115

**Kufanya mema:** “Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini na wakatenda mema ya kwamba Atawapa msamaha na thawabu kubwa.” Qur’an 5:9

## HITIMISHO

Kwa muhtasari, Qur’an inamfundisha mwanadamu jinsi ya kumuabudu Mungu Mmoja wa Kweli, hivyo kutimiza kusudi lao la kweli la maisha, na kupata mafanikio katika dunia hii na Akhera.

*“Hakika tumekuteremshia (Ewe Muhammad) Kitabu kwa ajili ya wanadamu kwa haki. Basi atakayeongoka ni kwa ajili ya nafsi yake, na atakayepotea basi amepotea kwa hasara yake mwenyewe.”*

Qur’an 39:41







**HOTLINE**  
 +971 56 204 2045  
 islamicicdxb

islamicic.com @ info@islamicic.com +971 4 355 5223

SCAN QR CODE FOR E-VERSION OF FLYER

iicdx.com/swahili

CONTENTS



سبيلك للسلام  
Your Path To Peace..  
**FREE COPY**



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

# YENYE KUFHAMIKA VIBAYA KUHUSU UISLAM

SWAHILI [06/10]

مفاهيم خاطئة حول الإسلام

ERRORISM HIJAB  
SWORD POETRY  
VIOLENCE MOON

GOD VALUES  
ARABS JIHAD  
OPPRESSION

*Kitu gani unachokijua  
kiukweli kuhusu  
Uislamu?*

PART OF



icelibrary.com | islamicic.com



دائرة الشؤون الإسلامية والعمل الخيري  
Islamic Affairs & Charitable Activities Department

# Utangulizi


Uislamu ni katika dini kubwa na zenye kuenea kwa kasi duniani, lakini ndio dini yenye kufahamika vibaya zaidi kwa sababu tofauti, ziwe za kisiasa, kiuchumi, matakwa ya vyombo vya habari au khofu ya mambo mengine. Mambo yasio ya kweli na mambo yenye utata yameenea kuhusu uislamu. Jambo la muhimu katika kuufahamu uislamu na waislamu ni kuwacha kuamini fikra zilizoenea na kuchunguza kila kitu kulingana na mafundisho ya uislamu na misingi sahihi ya uislam.

## 1. Waislamu hawawatakii kheri wasiokuwa waislamu, wala hawaishi nao kwa wema.

Wanazua baadhi ya watu kwamba mila za kiislamu haziendi sambamba na mila za kimagharibi, na uzushi huu uko mbali sana na ukweli.

Na tunasema hivi kwasababu waislamu wanazipenda mila nzuri za kidunia kama vile:

- Kuwa muaminifu na muadilifu
- Kuwa mwenye kuchunga miadi
- Kukubali uhuru wa kiitikadi
- Kuheshimu wazee wawili, na ndugu, na jirani, na mkubwa wako kwa miaka.
- Kutoa katika mambo ya kheri, kuwa mkarimu, na kusaidia mafakiri na wenye haja
- Na kuwafanyia wema jirani
- Kutodanganya, kutoghushi, wala kutukana au kusengenywa mtu yeyote.

















Na waislamu wanatakiwa kuisaidia jamii vizuri, na kuzilazimisha nafsi zao kuwa na tabia njema na kuzungumza maneno mazuri na kutenda matendo mema.

## 2. Waislamu wanamuabudu Mungu mpya anaeitwa "Allah".

Na neno "Allah" ni neno ambalo lina maana ya Mungu katika lugha ya kiarabu, na ndio neno lenye maana pana na ya dhati, lenye kumaanisha mola mmoja aliepwekeka. Na ndio neno wanalolitumia wakristo na mayahudi waarabu kuashiria neno "Mungu".

Japokuwa waislamu, mayahudi na wakristo wanamwamini Mungu huyo huyo (muumba) mmoja, lakini ufahamu wao kuhusu Mungu ni tofauti sana, kwa mfano waislamu





wanakataa kuwepo wazazi au watoto wa Mungu, au Mungu kuwa ni mmoja wa waungu watatu na wanaelekeza ukamilifu wote kwa Allah (mtukufu) pekee.

### 3. Uislamu unaruhusu ugaidi.

Vyombo vya habari vinajenga picha ya kwamba kila muislamu anaepigana kuwa ni gaidi, bila ya kujali kuwa anapigana katika haki au la, au kuwa yeye ndie anaekandamiza au anaekandamizwa.

Na Uislam unapinga sana kumpiga asiekuwa mpiganaji katika vita, waislamu hawaruhusiwi kuharibu miti na wanyama bila ya ruhusa, na kuwaacha watu wasio na hatia. Lakini ni muhimu kutofautisha baina na ugaidi na kukataa kutawaliwa, haya ni mambo mawili tofauti.

Na Uislamu umeweka wazi hatari ya kuua nafsi iliokatazwa kuuliwa, na imetilia umuhimu kuthamini maisha na watu:

*“(Kwamba) Atakaemuua mtu bila ya yeye kuua mtu, au bila ya kufanya ufisadi katika nchi basi ni kama alieua watu wote, na mwenye kumwacha hai mtu mmoja ni kama amewaacha hai watu wote”*

Al-Maidah 32

### 4. Uislam unamkandamiza mwanamke

Katika uislam wanaume na wanawake wako sawa mbele ya Allah, katika kupata thawabu na adhabu katika matendo yao na kwamba hakuna ubora wa mtu kwa mtu mwengine mbele ya Allah isipokuwa kwa uchamungu.


*“Kwa hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allah ni Yule amchae Mungu zaidi katika nyinyi”*







Al-Hujurat 13

Na aya hii inathibitisha kwamba utukufu wa kweli hauwi kwasababu ya ufakiri wa mtu au utajiri wake, na weusi na weupe wake, isipokuwa unakuja kwa uchamungu na ukweli, sawa sawa akiwa ni mwanamme au mwanamke.

Na uislamu umempa mwanamke heshima na haki zake zote, kama vile haki ya kulipa, haki ya kuchagua mchumba amtaxae, na kutafuta elimu, na kutaka kuachwa na haki ya kupata fungu lake katika mirathi.

Kwa masikitiko makubwa kuna baadhi ya wanawake wa kiislamu ambao wanakandamizwa na hawapewi haki zao. Na hii si aibu kwa uislam, lakini ni aibu ya baadhi ya nchi ambazo watu wanafuata mila na tamaduni ambazo hazina uhusiano na uislam.





## 5. Qur-an ni kitabu cha historia na ushairi.

Qur-an tukufu ni maneno ya Allah mtukufu, aliyomfunulia mtume Muhammad (amani ya Allah iwe juu yake). Nayo ni yenye kupambanua baina ya (haki) ukweli na (batili) uongo, na imekusanya misingi ya uongofu ambao watu wote wanautafuta.

Qur-an inaeleza mazingatio na masomo katika visa vya mitume iliopita na watu wao ili tujifunze kwa mfano wao.

Na vile vile Qur-an inatuhabarisha kuhusu Allah na kuhusu sisi wenyewe, na lengo la kuumbwa kwetu, ambako ni kumtambua na kumpwekesha Allah, mola wa walimwengu wote.

Kwa hakika Allah hakutuumba bure na hakutuacha bila mwelekeo. Na kujaribiwa imani ya mja ni katika kuitumia akili yake, matakwa yake, na fikra zake na ili aongoke kwa

kuvitumia vitu hivyo ili atambue uwepo wa mola muumba- na moja katika dalili kubwa (za uwepo wa Allah) ni Quran Qur-an imekusanya miujiza mengi ili (ituthibitishie, na) tusiwe na shaka kwamba inatoka kwa mola muumba wa ardhi na mbingu.

*Na njia bora ya kuijua Qur-an inazungumzia nini ni kuisoma wewe mwenyewe.*

## 6. Hijab ni jambo la kumkandamiza mwanamke.

Tuiangalie Hijab kwa mazingatio, kwani waislamu wanawake wameamrisha kufunika miili yao kwa mavazi mema na wasidhihirishe mapambambo yao kwa wasiokuwa maharimu wao katika wanaume.

Na hijabu sio vazi la nje pekee, kwa hakika hijab ni kuzungumza maneno mazuri, na vile vile kuwa tabia njema.








Japokuwa kuna faida nyingi za hijab, sababu kuu ya wanawake wa kiislamu kuchunga hijab ni kwasababu ni amri kutoka kwa Allah na yeye ni mjuzi wa yalio bora na yanayowafaa waja wake.

Kwa hakika hijab inamtukuza mwanamke kwa kutilia mkazo uzuri wake wa ndani /wa kiroho baada ya kuona uzuri wake wa nje. Nayo (hijab) inawapa uhuru wanawake kuwa washiriki wazuri katika jamii zao, hapo hapo huweza kulinda heshima zao.

Hijab haiashirii unyanyasaji au ukandamizaji, lakini ni ngao dhidi ya kudharaulika, na kutengwa bila ya haki. Kwahiyo mara nyengine utakapomuona mwanamke muislamu, fahamu ya kwamba anachokifunika ni umbile lake sio akili yake.

## 7. Waislamu wote ni waarabu

Ukweli hauko hivyo, asilimia 20% tu ya waislamu ndio waarabu, maana yake ni kwamba asilimia 80% ya waislamu, si waarabu. Kwa mfano kuna wahindi waindonesia ambao ni waislamu kuliko waislamu waarabu.



Na katika mafundisho ya uislamu ni kwamba hakuna ubora wa mtu kwasababu ya rangi yake, na uislamu umepinga sana ubaguzi wa rangi. Uislamu una ujumbe kwa watu wote, kwamba kila mmoja apate amani na mafanikio kwa kumwamini Mungu wa kweli mmoja tu ambae ni “Allah”.

### 8. Jihad ni Ugaidi

Maana halisi ya neno “Jihad” ni kupigania na kujitolea mtu kwa ajili ya dini yake katika namna ambayo inamridhisha Allah. Kilugha neno “jihad” lina maana ya “kupigania” na ina maana mtu apiganie kufanya matendo mema, kuchangia mambo ya kheri au kuunda nguvu moja kazi ya jeshi la kiislamu. Maana maarufu ya neno Jihad ni hii ya jeshi la kiislamu ambayo imeruhusiwa kwa ajili ya kulinda ustawi wa jamii na kulinda kutoenea unyanyasaji na kulinda haki. Lakini hii inaweza kuwa ulinzi au hujuma inategemea na hali.

### 9. Waislamu wanamuabudu Muhammad au Mungu wa mwezi

Vile vile jambo jengine lenye kufahamika vibaya ni kwamba waislamu wanamuabudu mtume Muhammad (amani ya Allah iwe juu yake). Hili si jambo la kweli kabisa, na inathibitishwa na kauli ya mtume “Musichupe mpaka katika kunisifu, kama walivyochupa mipaka manasra katika kumsifu Issa bin Maryam, kwa hakika mimi ni mja , basi semeni mja wa Allah na mtume wake” bukhari (3445)

*Kwa hakika katika mafundisho ya Qur-an ni kuwaheshimu mitume wote, lakini kuwaheshimu na kuwapenda haimaanishi ndio tunawaabudu.*

Vile vile kuna uzushi kwamba waislamu wanaabudu “mungu wa mwezi” jambo ambalo sio sahihi kabisa. Katika Uislamu, kuabudia mwezi, au chochote ambacho sio Allah kumekatazwa sana na ni shirki.

*Amesema Allah mtukufu “basi msisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Allah alieviumba ikiwa nyinyi kweli mnamwabudu yeye(basi fanyeni hivi)”.*

Fuswilat:37

Uislamu unatambua ukamilifu, ukubwa na upekee wa Allah bila ya ujanja wowote. Basi yeye ni mola wa uadilifu na rehema. Kumwabudu Allah pekee ndio jambo la muhimu zaidi katika Uislamu, kama ilivyotajwa katika maneno ya Allah (katika sehemu tofauti ndani ya Qur-an).

### 10. Uislamu unaruhusu ndoa za kulazimishana

Ndoa za kupangwa (kuwalazimisha watoto kuoana) ni katika mila za baadhi ya nchi duniani. Japokuwa hazikukatazwa kwa waislamu lakini ndoa hizi zinahusishwa vibaya na Uislamu.




Na katika Uislam, mwanamme na mwanamke wana haki ya kuchagua au kukataa mchumba. Mtume Muhammad (amani ya Allah iwe juu yake) “Mjane ana haki zaidi kwa nafsi yake kuliko (haki alionayo) walii wake, na (mwanamke) bikira ashauriwe, na idhini yake ni kimya chake” (Muslim 1421)

## 11. “Uislam unawalazimisha watu kuwa waislamu”

Japokuwa ni wajibu kwa waislamu kufikisha ujumbe wa Uislam kwa wengine, lakini hakuna atakaelazimishwa kukubali Uislam. Mtu mwenyewe kwa nafsi yake na bila ya kulazimishwa aamini na amtii Allah, hivyo hakuna mtu atakaelazimishwa kukubali Uislam.

Zingatia mambo yafuatayo:

- Indonesia ina waislamu wengi zaidi lakini hakuna vita vilivyopiganwa kuleta Uislam katika nchi hii.
- Inafikia idadi ya warabu milioni 14 ambao ni wakristo na wameishi na wanaendelea kuishi katikamoyo wa kisiwa cha waarabu kwa miaka mingi sasa.
- Uislamu ndio dini inayoenea kwa haraka sana katika nchi za kimagharibi siku hizi.
- Japokuwa kupinga ukandamizaji na kutaka haki ndio sababu kubwa za Jihad, kuwalazimisha watu kukubali uislam si katika sababu za kisheria za Jihad katika uislam.
- Waislamu wameitawala Spain kwa miaka 800 lakini hakuna watu waliolazimishwa kutoka katika dini zao na kuingia katika uislamu.



## Hitimisho





Kujifunza Uislam kutoka vyanzo vibaya ni hatari na vinapelekea kuufahamu vibaya Uislam. Usiongozwe vibaya kwa kukubali mambo yasiosahihi na habari za uongo kuhusu uislam – imani inayofuatwa na zaidi ya robo ya watu wote duniani.

Je! Ujumbe wa Uislam ambao ni muongozo kwa watu wote hautakiwi kupokewa na kuchunguzwa kwa umakini mkubwa?

**HOTLINE**  
 +971 56 204 2045  
 islamicicdxb

islamicic.com @ info@islamicic.com +971 4 355 5223

CONTENTS



سبيلك للسلام  
Your Path To Peace..  
**FREE COPY**



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

# HAKI ZA WANAWAKE katika UISLAMU

SWAHILI [07/10]

حقوق المرأة في الإسلام

*Kuheshimiwa... Kuthaminiwa...  
Kupendwa...*

PART OF




icelibrary.com | islamicic.com



دائرة الشؤون الإسلامية والعمل الخيري  
Islamic Affairs & Charitable Activities Department

# UTANGULIZI

Wanawake katika Uislamu hufikiwa kuwa wananyaswa, kudharauliwa, kukandamizwa - lakini je, ni kweli? Je, mamilioni ya Waislamu ni wakandamizaji kiasi hicho au haya ni mawazo potofu yaliyotengenezwa na vyombo vya habari vyenye upendeleo?



Zaidi ya miaka elfu moja mia nne iliyopita, Uislamu uliwapa wanawake haki ambazo wanawake katika Magharibi wameanza kuzifurahia hivi karibuni tu. Katika miaka ya 1930, Annie Besant aliona, “Ni katika miaka ishirini tu iliyopita ambapo Uingereza ya Kikristo imetambua haki ya mwanamke kumiliki mali, wakati Uislamu umetoa haki hii tangu zamani. Ni kashfa kusema kwamba Uislamu unafundisha kwamba wanawake hawana roho.” (Maisha na Mafundisho ya Muhammad, 1932).

Wanaume na wanawake wote walitokana na mtu mmoja - Nabii Adam (amani iwe juu yake). Uislamu haukubali kwa yeyote kati yao chochote isipokuwa haki na maamiliano ya huruma.

# MALIPO SAWA & UWAJIBIKAJI

Sawa Wanaume na wanawake humwabudu Allah kwa njia ile ile, maana wanamwabudu Mungu yule yule (Allah), hufanya matendo yale yale ya ibada, hufuata maandiko yale yale, na kushikilia imani zile zile. Allah (neni la Kiarabu kwa Mungu wa kweli wa uumbaji wote), Huhukumu wanadamu wote kwa haki na usawa. Allah Anasisitiza maamiliano ya haki na malipo yanayostahili kwa wanaume na wanawake katika aya nyingi za Qur'an:

*“Allah Amewaahidi waumini, wanaume na wanawake, bustani zipitazo mito chini yake, watakaa humo, na majumba mazuri katika bustani za neema ya milele.”*








**Qur'an 9:72**

*“Sitaipoteza tendo la mtendaji yeyote kati yenu, mwanaume au mwanamke; nyinyi ni kutoka kwa kila mmoja.”*

**Qur'an 3:195**

Aya hizi zinaonyesha kwamba malipo yanategemea matendo ya mtu na siyo jinsia yake. Jinsia haina nafasi yoyote katika jinsi mtu anavyolipwa na kuhukumiwa.





Tukilinganisha Uislamu na dini nyingine, tunaona kwamba inatoa haki kati ya jinsia. Kwa mfano, Uislamu unakataa wazo kwamba Hawa ndiye mwenye hatia zaidi kuliko Adam kwa kula kutoka kwenye mti ulioharamishwa. Kulingana na Uislamu, Adam na Hawa wote walikosea, wote walitubu na Mungu Aliwasamehe wote.

## HAKI SAWA YA KUPATA ELIMU

Wanaume na wanawake wote wanahimizwa kwa usawa kutafuta elimu. Nabii (amani iwe juu yake) alisema, “Elimu ni lazima kwa kila Muislamu.”

Pia, walikuwepo wasomi wakubwa wa Kiislamu wa kike wakati karibu na wakati wa Nabii (amani iwe juu yake). Baadhi walikuwa kutoka familia yake na wengine walikuwa maswahaba wake au binti zao. Maarufu kati yao alikuwa Aisha, mke wa Nabii (amani iwe juu yake) ambaye kupitia kwake robo ya sheria ya Kiislamu imenukuliwa.

Wanawake wengine walikuwa wasomi wakubwa wa fiqhi na walikuwa na wanafunzi mashuhuri wa kiume.

## HAKI SAWA YA KUCHAGUA MWENZA WA NDOA

Uislamu umewaheshimu wanawake kwa kuwapa haki ya kuchagua mwenza wa ndoa na kuhifadhi jina lao la familia ya asili baada ya kuolewa. Zaidi ya hayo, wengi wana dhana kwamba wazazi huwalazimisha binti zao kuolewa. Hii ni desturi ya kitamaduni, na haina msingi wowote katika Uislamu. Kwa kweli, ni marufuku.








Wakati wa Nabii Muhammad (amani iwe juu yake), mwanamke mmoja alimjia na kusema, “Baba yangu ameniozesha kwa binamu yangu ili kuinua hadhi yake ya kijamii na nililazimishwa.” Nabii alimtuma baba wa msichana huyo na kisha mbele yake akampa msichana huyo chaguo la kubaki kwenye ndoa au kuivunja. Alijibu, “Ewe Mjumbe wa Allah, nimekubali alichofanya baba yangu, lakini nilitaka kuonyesha wanawake wengine (kwamba hawawezi kulazimishwa kuolewa).”

## SAWA LAKINI TOFAUTI

Wakati wanaume na wanawake wana haki sawa kama kanuni ya jumla, haki na majukumu maalum waliyopewa siyo sawa. Wanaume na wanawake wana haki na majukumu yanayokamilishana.



# UPENDO NA REHEMA KATIKA MAHUSIANO YA NDOA



*“Na katika Ishara Zake ni kuwa Ameumba wake zenu kutoka kwenu ili mpate utulivu kwao; Naye Ameweka mapenzi na rehemu baina yenu. Hakika katika haya kuna Ishara kwa watu wanaofikiri.”*

**Qur'an 30:21**

Mtume (amani iwe juu yake) pia aliwahimiza wanaume kuwaheshimu wake zao kwa njia bora, “Bora wenu ni wale walio bora kwa wake zao.” Ameipokea Tirmidhi (3895).

Aisha (mke wa Mtume) aliulizwa kuhusu tabia ya Mtume akiwa nyumbani. Akasema, “Alikuwa kama mmoja wenu nyumbani, lakini alikuwa mpole sana na mkarimu sana... Alikuwa tayari

kusaidia wake zake katika kazi za kawaida za nyumbani, [alikuwa] anashona nguo zake mwenyewe na kushona viatu vyake.” Kwa ujumla, alisaidia katika kazi zote walizokuwa wakizifanya wake zake.

# HADHI TUKUFU YA MAMA NA MABINTI

Mama ana ushawishi mkubwa kwa mtoto hasa katika miaka ya awali kupitia upendo wake, huruma na malezi. Bila shaka, mafanikio ya jamii yanatokana na kina mama. Kwa hiyo, ni haki kabisa kwa Uislamu kuwaheshimu na kuinua hadhi yao.

Allah anasema katika Qur'an:








Mtume (amani iwe juu yake) aliulizwa, “Ewe Mtume wa Allah, nani kati ya watu anastahili matendo yangu mema zaidi?”

Akasema, “Mama yako.” Mtu huyo aliuliza mara nyingine, “Kisha nani?” Akasema, “Mama yako.” Akarudia mara ya tatu na akajibiwa vilevile. Ni hadi mara ya nne ndipo Mtume akasema, “Kisha baba yako.”

*“Na Tumemuusia mwanadamu kuwafanyia wema wazazi wake. Mama yake amembeba tumboni kwa shida, na akamzaa kwa shida.”*

**Qur'an 46:15**

Thawabu haitolewi tu kwa kutenda wema kwa mama. Kwa hakika, Uislamu umeweka thawabu maalum kwa kulea mabinti ambayo haitolewi kwa kulea wana.



Mtume Muhammad (amani iwe juu yake) alisema, “Yeyote ambaye Allah Amemruzuku mabinti wawili na akawafanyia wema, watakuwa sababu ya yeye kuingia Peponi.”

# HITIMISHO

Kabla ya Uislamu, wanawake walionekana kuwa aibu, watoto wa kike walizikwa wakiwa hai, ukahaba ulikithiri, talaka ilikuwa mikononi mwa mwanaume tu, urithi ulikuwa kwa wenye nguvu tu, na dhuluma ilienea. Uislamu ulipoingia uliondoa vitendo hivi. Hata sasa, katika “nchi zilizoendelea”, wanawake hawapewi heshima, hadhi na taadhima wanayostahili, achilia mbali malipo sawa kwa kazi sawa. Uislamu, hata hivyo, unawaona wanawake kuwa wa thamani na wa heshima, si watu wa kudharauliwa au kubezwa. Uonevu dhidi ya wanawake katika baadhi ya nchi za Kiarabu au familia za Kiislamu hutokana na mila za kitamaduni ambazo baadhi ya Waislamu huzifuata kimakosa, si kwa sababu ya Uislamu. Mbona basi wanawake wengi duniani huingia katika Uislamu kwa hiari yao kama ni dini ya kuwanyanyasa?








Tunamaliza kwa maneno ya Mola wetu na Mola wenu, Muumba na Mruzuku wa wanaume na wanawake wote:

*“Hakika Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, na Waumini wanaume na Waumini wanawake, na watiifu wanaume na watiifu wanawake, na wasemao kweli wanaume na wanawake, na wenye subira wanaume na wanawake, na wanyenyekevu wanaume na wanawake... Allah amewaandalia msamaha na thawabu kubwa.”*

**Qur'an 33:35**

**HOTLINE**  
 +971 56 204 2045  
 islamicicdx

islamicic.com @ info@islamicic.com +971 4 355 5223



سبيلك للسلام  
Your Path To Peace...  
**FREE COPY**



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

# Miujiza ya Kielimu ya QUR'AN

SWAHILI [08/10]

الإعجاز العلمي في القرآن

“  
Tutawaonyesha ishara  
Zetu katika ulimwengu na  
ndani ya nafsi zao, mpaka  
iwadhahirikie kwamba  
huu ni ukweli.”  
[Qur'an 41:53]






PART OF



icelibrary.com | islamicic.com




دائرة الشؤون الإسلامية والعمل الخيري  
Islamic Affairs & Charitable Activities Department



Qur'an, kitabu cha Uislamu, ni kitabu cha mwisho cha ufunuo kutoka kwa Mungu kwa wanadamu, na cha mwisho katika mlolongo wa vitabu vilivyoteremshwa kwa Manab'ii.

Ingawa Qur'an (iliyoteremshwa zaidi ya miaka 1400 iliyopita) si kitabu cha sayansi, inabeba dalili kuhusu ukweli wa kisayansi ambao umegunduliwa hivi karibuni kutokana na maendeleo ya teknolojia na maarifa ya kisayansi. Uislamu unahimiza tafakari na utafiti wa kisayansi, kwa sababu kuelewa maumbile ya uumbaji kunamuwezesha mtu kumheshimu zaidi Muumba wake na kuelewa ukubwa wa nguvu na hekima Yake.

Qur'an iliteremshwa katika zama ambapo sayansi ilikuwa bado ni ya awali; hakukuwa na darubini, hadubini wala teknolojia ya kisasa kama leo. Watu waliamini kuwa jua linazunguka dunia na kwamba mbingu zimeshikwa na nguzo pembezoni mwa dunia tambarare. Katika muktadha huo, Qur'an iliteremshwa ikibeba ishara za ukweli mwingi wa kisayansi kuanzia astronomia, biolojia, jiolojia, hadi elimu ya wanyama.



Baadhi ya ukweli wa kisayansi unaopatikana katika Qur'an ni kama ifuatavyo:

## 1 - ASILI YA UHAI

Maji yanaonyeshwa kuwa chanzo cha kila kiumbe hai. Viumbe vyote vinaundwa na seli, na sasa tunajua kuwa seli nyingi zina maji.

Hili liligunduliwa baada ya kuvumbuliwa kwa hadubini. Katika jangwa la Arabia, haingekuwa rahisi mtu kudhani kuwa maisha yote yanatokana na maji.

## 2 - UKUAJI WA KIJUSI CHA BINADAMU

Mungu anazungumzia hatua za maendeleo ya kijusi cha mwanadamu:

*"Tumemuumba mwanadamu kutoka kwenye kiini cha udongo, kisha tukamuweka kama tone katika mahali palipolindwa, kisha tukaligeuza tone hilo kuwa alaqah (kiumbe kinachoning'inia, kama funza, au kigandamizo cha damu), kisha tukaligeuza kuwa mudghah (kitu kama cha kutafunwa)..."*

[Qur'an 23:12-14]

Neno la Kiarabu "alaqah" lina maana tatu: funza, kitu kilichoning'inia, na kigandamizo cha damu. "Mudghah" maana yake ni kitu kama cha kutafunwa. Wanasayansi wa embryolojia wamegundua kuwa maelezo haya yanaendana kikamilifu na sayansi ya kisasa.

### 3 - UPANUZI WA ULIMWENGU

Katika wakati ambapo elimu ya nyota ilikuwa bado ni ya awali, Qur'an ilisema:

*“Na mbingu tumeziumba kwa nguvu, na kwa hakika Sisi ndio tunaopanua.”*

[Qur'an 51:47]

Katika maana makusudiwa ya ayah iliyojuu ni kwamba Mungu Mwenyezi Anaipanua ulimwengu (ai. mambingu). Maana zengine ni kwamba Mwenyezi Mungu Yuwaruzuku, Ana nguvu juu ya, ulimwengu - ambayo pia ni kweli.

Ugunduzi huu ulifanyika katika karne iliyopita. Mwanafizikia Stephen Hawking alisema: “Ugunduzi kwamba ulimwengu unapanuka ulikuwa ni moja ya mapinduzi makubwa ya akili ya karne ya ishirini.”

Qur'an inaashiria kwa kupanuka kwa ulimwengu hata kabla ya kuvumbiwa kwa darubini!

### 4 - KUSHUSHWA KWA CHUMA

Chuma hakikutokana na ardhi, bali kilikuja kutoka anga za mbali kupitia miamba ya angani. Wanasayansi waligundua kwamba mabilioni ya miaka iliyopita, kwamba ardhi iligongwa na vimondo vidogo vilivyo beba chuma toka kwa nyota mbali iliyolipuka.

Mwenyezi Mungu Atumia maneno 'teremsha'. Kuna rai ya kisayansi yenye nguvu ielezayo kwa kuteremshwa kwa chuma toka anga za mbali kupitia kwa vimondo vidogo vilivyoanguka, maelezo ambayo hayakuweza kujulikana na sayansi changa ya karne la saba.

*“Na tumeteremsha chuma kikawa na nguvu nyingi na manufaa kwa wanadamu.”*

[Qur'an 57:25]

### 5 - ULINZI WA ANGA







Anga ina kazi muhimu ya kulinda ardhi na wakazi wake kutoka na miale yenye kuu ya jua, pamoja na ubaridi mkali wa anga ya mbali.

Mungu Mwenyezi Anatuamrisha tuzingatie anga kwa ayah ifuatayo:

*“Na tumefanya mbingu kuwa dari la ulinzi, lakini wao wanazikataa ishara Zetu.”*

[Qur'an 21:32]

Qur'an inaashiria kwa ulinzi wa anga kuwa dalili ya Uwezo wa Mungu Mwenyezi, sifa za ulinzi zilizogunduliwa kwa utafiti wa kisayansi uliyojiri karne la ishirini.



## 6 - MILIMA


Mungu Mwenyezi Anatuelekeza kwa sifa muhimu ya milima:

*“Je! Hatukufanya ardhi kuwa mahali pa kupumzika na milima kuwa kama vigingi?”*

[Qur'an 78:6-7]

Qur'an inaeleza kwa usahihi mizizi mirefu ya milima kwa kutumia neno “vigingi”. Mlima Everest, kwa mfano, una urefu wa takriban km 9 juu ya ardhi, ilhali mzizi wake unaenda chini zaidi ya km 125!

Ukweli kwamba milima ina mizizi mirefu kama vigingi haukujulikana hadi baada ya kugunduliwa kwa nadharia ya miendo ya sahani za ardhi mwanzoni mwa karne ya ishirini. Mungu pia anasema katika Qur'an (16:15), kwamba milima ina jukumu la kuistahimili ardhi “...ili isitikisike,” jambo ambalo limeanza tu kueleweka na wanasayansi.



## 7 - MZUNGUKO WA JUA








Mnamo mwaka 1512, mwanaastronomia Nicholas Copernicus alitoa nadharia yake kuwa Jua haliamishiki na liko katikati ya mfumo wa jua, na sayari huzunguka kulizunguka. Imani hii ilikuwa imeenea sana miongoni mwa wanaastronomia hadi karne ya ishirini. Sasa ni ukweli ulio thibitishwa kuwa Jua halisimami, bali linazunguka katika mzunguko kuzunguka kitovu cha galaksi yetu ya Njia ya Maziwa (Milky Way).

*“Yeye ndiye aliyeumba usiku na mchana, na Jua na Mwezi, vyote vikiwa vinaelea katika mzunguko wake.”*

[Qur'an 21:33]

## 8 - MAWIMBI YA NDANI BAHARINI

Ilikuwa inafikiriwa kuwa mawimbi hutokea tu juu ya uso wa bahari. Hata hivyo, wanasayansi wa bahari wamegundua kuwa kuna mawimbi ya ndani yanayotokea chini ya uso wa bahari ambayo hayaonekani kwa macho ya kawaida na yanaweza kugunduliwa tu kwa kutumia vifaa maalumu.



Qur'an inataja:

*"... bahari kubwa iliyofunikwa na mawimbi, juu yake yapo mawimbi, juu yake yapo mawingu, giza juu ya giza..."*

[Qur'an 24:40]

Maelezo haya ni ya kushangaza kwa sababu miaka 1400 iliyopita hakukuwa na vifaa maalum vya kugundua mawimbi ya ndani ya bahari.

## 9 - UONGO NA HARAKATI

Alikuwepo kiongozi mmoja wa kikabila dhalimu na mjeuri aliyekuwa akiishi wakati wa Mtume Muhammad (rehma na amani ziwe juu yake). Mungu aliteremsha aya kumuonya:

*"Hapana! Kama hatakoma, hakika tutamshika kwa kipaji cha uso wake; kipaji chake cha uongo na dhambi."*

[Qur'an 96:15-16]

Mungu hamwiti mtu huyo mwongo, bali anaita kipaji cha uso wake (sehemu ya mbele ya ubongo) kuwa "cha uongo" na "cha dhambi," na anamwonya aache. Tafiti nyingi zimeonyesha kuwa sehemu ya mbele ya

ubongo (frontal lobe) inahusika na uongo na harakati za hiari, na hivyo pia na dhambi. Vipengele hivi viligunduliwa kwa kutumia vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa ubongo vilivyotengenezwa katika karne ya ishirini.









## 10 - BAHARI MBILI ZINAZOKUTANA BILA KUCHANGANYIKA

Kuhusu bahari, Muumba wetu anasema:

Nguvu ya kimwili iitwayo mvutano wa uso (surface tension) huzuia maji ya bahari zinazokaribiana kuchanganyika, kwa sababu ya tofauti ya msongamano wa maji haya. Ni kana kwamba kuna ukuta mwembamba kati yao. Hili limegunduliwa hivi karibuni tu na wanasayansi wa bahari.

*"Ameyaacha bahari mbili zikikutana, baina yao kuna kizuizi ambacho hawakivuki."*

[Qur'an 55:19-20]



# JE, MUHAMMAD ANGEWEZA KUANDIKA QUR'AN?


Mtume Muhammad (rehma na amani ziwe juu yake) alijulikana katika historia kuwa hakuwa na elimu ya kusoma wala kuandika na hakuwa na elimu yoyote ya kitaaluma inayoweza kueleza usahihi wa kisayansi uliopo katika Qur'an.

Wengine wanaweza kudai kwamba aliinakili kutoka kwa watu waliokuwa na elimu au wanasayansi wa wakati wake. Kama, tungetarajia kuona pia makosa yote ya kisayansi yaliyokuwepo wakati huo. Kinyume chake, tunaona kuwa Qur'an haina makosa yoyote - iwe ya kisayansi au vinginevyo.

Watu wengine pia wanaweza kudai kwamba Qur'an ilibadilishwa kadiri ukweli wa kisayansi ulivyogunduliwa. Hili haliwezekani kwa sababu ni jambo lililowekwa kihistoria kuwa Qur'an imehifadhiwa katika lugha yake ya asili - jambo ambalo lenyewe ni muujiza!








# JE, NI SUDFA TU?

Ingawa kijitabu hiki kimezingatia zaidi miujiza inayohusiana na sayansi, kuna aina nyingine nyingi za miujiza yaliyothibitishwa yaliyotajwa katika Qur'an: miujiza ya kihistoria; unabii uliotimia; mtindo wa lugha na fasihi usiolinganishwa; na pia athari kubwa inayopatikana ndani ya mioyo ya watu. Miujiza hii yote haiwezi kuwa kwa bahati tu. Inathibitisha wazi kuwa Qur'an ni kutoka kwa Mungu, Muumba wa sheria hizi zote za kisayansi. Yeye ndiye Mungu mmoja aliyewatuma Manabii wote kwa ujumbe mmoja - kumwabudu Mungu mmoja tu na kufuata mafundisho ya Mtume Wake.



Qur'an ni kitabu cha mwongozo kinachothibitisha kuwa Mungu hakuumba binadamu ili waishi bila lengo. Bali, inafundisha kuwa tuna lengo la juu na lenye maana katika maisha - kulitambua ukamilifu, ukuu na upekee wa Mungu, na kumtii.









Ni juu ya kila mtu kutumia akili na uwezo wa kufikiri aliopewa na Mungu ili kutafakari na kutambua Ishara za Mungu - Qur'an ikiwa ni Ishara muhimu zaidi. Soma na ugundue uzuri na ukweli wa Qur'an, ili upate mafanikio!



**HOTLINE**  
 +971 56 204 2045  
 islamicicdxb

islamicic.com | info@islamicic.com | +971 4 355 5223

SCAN QR CODE FOR E-VERSION OF FLYER | iicdx.com/swahili



سبيلك للسلام  
Your Path To Peace...  
**FREE COPY**



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

# KIFO *na* MAISHA YA BAADA YA KIFO *katika* UISLAMU

SWAHILI [09/10]

الموت والآخرة في الإسلام

*“Kila nafsi itaonja mauti.”*

Qur'an 29:57








PART OF



[icelibrary.com](http://icelibrary.com) | [islamicic.com](http://islamicic.com)




دائرة الشؤون الإسلامية والعمل الخيري | Islamic Affairs & Charitable Activities Department  
(2017/139)



# KIFO KIKO KARIBU

Kifo ni ukweli ambao hakuna mtu anayeweza kukiepuka. Kinakaribia kila siku; kila saa; kila dakika. Kulingana na The World Factbook ya CIA ya mwaka 2007, karibu watu wawili hufariki kila sekunde. Hiyo ni jumla ya kushangaza ya watu milioni 57.9 kila mwaka! Kila kiumbe mmoja mmoja atafikia hatima hii isiyozuilika, bila kujali umri wao, afya, asili, hali ya kijamii au uchamungu.



Wako wapi wafalme wa zamani, mabilionea na wenye nguvu? Wako wapi waliokuwa wazuri wa sura, mashuhuri, na wasomi wa juu?

# UHALISIA WA KIFO

Kifo si msiba, bali ni kupita kutoka katika dunia hii kwenda maisha mengine. Kinapaswa kutufanya tutafakari na kuwaza juu ya madhumuni ya maisha, na nini kitatupata baada ya kifo.

Allah (Mungu) Ametufahamisha katika Qur'an kuwa Ametuumba kwa madhumuni ya kumuabudu Yeye peke Yake na kwamba Amefanya maisha haya kuwa mtihani ili kuona ni nani atayatimiza madhumuni hayo makuu:

*“Na Sikuumba majini na watu ila waniabudu Mimi.”*

Qur'an 51:66

Mungu pia Ametufahamisha sababu ya kuumbwa kwa kifo na uhai:

*“Yeye Ndiye Aliyekuumbieni mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mzuri kwa vitendo.”*

Qur'an 67:2

Mtu haandai kifo kwa kulipia huduma za mazishi mapema au kuchagua jeneza kabla ya wakati. Ni kuhusu kutimiza madhumuni ya maisha – kumuabudu Allah peke Yake, kuishi kulingana na maamrisha Yake, na kutenda mema. Dhana ya ibada katika Uislamu ni pana na si tu kuswali. Kwa hakika, tendo lolote linalompendeza Allah huhesabiwa kuwa ni ibada, na mtu hulipwa thawabu kwa hilo duniani au Akhera.

# WAKATI WA KIFO

Kila siku tunaona mifano ya kifo. Tunaona kifo cha amani kama kile kisicho na maumivu wala vurugu. Hata hivyo, si lazima iwe hivyo. Mtu anapokufa, roho hutoka mwilini, na hivyo sura ya mwili huenda isioneshe hali ya roho. Amani au taabu ya roho itakuwa ni matokeo ya moja kwa moja ya jinsi mtu alivyoitimiza madhumuni yake katika maisha haya, na si kuhusu chanzo cha kifo.

*“Kila mtu na aangalie amekitanguliza nini kwa ajili ya kesho.”*

**Qur'an 59:18**

Fikiria mfano wa watu wawili waliopata tiketi ya njia moja kwenda sehemu wasiyoijua. Mtu wa kwanza anachukua muda kujifunza lugha, utamaduni na mienendo ya sehemu hiyo. Anapata sarafu sahihi na chanjo, na wakati wa safari ukifika, anawasili bila mshangao. Yuko salama na mwenye furaha, kwa sababu amejiaandaa vizuri.

Kwa upande mwingine, mtu wa pili ni mzembe katika maandalizi yake na huishi kwa kufurahia muda tu hadi wakati wa kuondoka unapofika. Anawasili sehemu isiyojulikana akiwa na hofu na kuchanganyikiwa. Kutokujitayarisha kwake kunamsababisha kupata hatima mbaya, kwani vitu vyote alivyobeba havikumfaa.

Kumuelezea mtu wa namna hiyo, Allah anasema katika Qur'an:

*“Mpaka mauti yanapomjia mmoja wao, husema: ‘Mola wangu nirudishe nyuma! Ili nifanye mema katika yale niliyoyaacha.’ Hapana! Haya ni maneno tu anayoyasema.”*








**Qur'an 23:99-100**

Pia zingatia majibu ya wale waliotupwa Motoni, wanapoulizwa nini kiliwapelekea huko:

*“Watasema, ‘Sisi hatukuwa miongoni mwa waliokuwa wakiswali. Wala hatukuwalisha masikini. Na tulikuwa tukizungumzia mambo ya upuuzi pamoja na wenye kufanya hivyo, na tulikuwa tukikanusha Siku ya Malipo (Siku ya Hukumu), mpaka yakatujia yale yaliyokuwa yakini (kifo).’ ”*

**Qur'an 74:43-47**

Sote tuna wakati uliopangwa wa kufa, na sote tutaelekea katika sehemu hii isiyojulikana. Jiulize – je, umejiandaa kwa safari hiyo?



# MADHUMUNI YA MAISHA

Maisha ni mtihani unaomalizika kwa kifo, lakini hakimaanishi mwisho wa kuwepo kwa mtu. Kifo kikishafika, fursa ya kutenda mema hufikia tamati. Itakuwa ni kuchelewa kutubu, na hatima yetu itaamuliwa na imani zetu na matendo yetu katika maisha haya ya sasa. Maisha ya mwanadamu yamegawanyika katika sehemu mbili: maisha mafupi hapa duniani, na maisha ya milele ya baadaye. Akili yoyote timamu itakubali kuwa neema ya milele ni bora zaidi kuliko starehe fupi za duniani. Allah Alimuumba mwanadamu na Akamfanya kuwajibika kwa matendo yake kwa kumpa uhuru wa kuchagua, na akili ya kutofautisha mema na mabaya. Kama kusingekuwepo na maisha ya baadaye ambako wema wangelipwa na waovu kuadhibiwa, hilo lingekinzana na haki kamilifu ya Allah. Kwa hivyo, ni hitaji la haki kamili kuwa kuwe na Siku ya Hukumu ambayo kila roho italetwa kuhesabiwa.

“Je, mlidhani kuwa Sisi (Mungu) tuliwaumba kwa mchezo (bila madhumuni yoyote), na kwamba hamtarudishwa kwetu (Mungu)?”

Qur'an 23:115

“Je, Sisi tutawafanya Watu wa Imani sawa na Watu wa Dhambi? Mna nini? Mnahukumu vipi?”

Qur'an 68:35-36

# SIKU YA HUKUMU








Matendo ya kila mtu katika maisha haya yameandikwa kwa usahihi na kuhifadhiwa, kama Allah asemavyo:








“Na Kitabu (cha Matendo) kitawekwa wazi, na utaona wakosefu wakiwa katika hofu kubwa kwa yaliyomo ndani yake. Watasema, ‘Ole wetu! Kitabu gani hiki hakiachi dogo wala kubwa ila kimetaja!’ Nao watakuta yote waliyoyatenda yamewekwa mbele yao. Na Mola wako hatendi dhuluma kwa yeyote.”

“Sema, kifo mnachokikimbia, hakika kitakupateni. Kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri (yaani Allah), Naye Atawajulisheni mliyoyatenda.”

Qur'an 62:8

Qur'an 18:49





Tutashangazwa na Usahihi wa Rekodi ya Matendo Yetu, kwani tutakumbushwa mambo ambayo tuliyasahau kabisa. Allah Anasema:

*“Allah Ameyahifadhi (matendo yao), ilhali wao wameyasahau.”*

**Qur'an 58:6**

Kutafakari kwa kina juu ya hili kunapaswa kutufanya tuone haya kutenda dhambi yoyote tukijua kuwa itarekodiwa dhidi yetu na kufichuliwa Siku ya Hukumu mbele ya Allah.

Kwa wale wanaotia shaka uwezo wa Allah wa kuhuisha wafu na kuwahukumu, Allah Ananukuu makafiri wakisema:

*“Ni nani atakayehuisha mifupa hii iliyo oza na kuwa mavumbi?’ Sema (Ewe Muhammad), ‘Ataifufua Yeye Aliyeiumba mara ya kwanza! Naye ni Mjuzi wa kila kiumbe!’ ”*

**Qur'an 36:78-79**

## PEPONI NA MOTONI

Wale wanaomuamini Allah kama Mungu wa pekee anayestahiki kuabudiwa, na wakatenda mema, watapata malipo ya Pepo.


Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amesimulia kuwa Allah amesema:

“Nimewaandalia waja Wangu wema mambo mazuri mno ambayo jicho halijawahi kuyaona, wala sikio kusikia, wala moyo wa binadamu kufikiria.”

Hili linatofautiana kabisa na watu wanaokataa Umoja wa Allah, ambao wataambiwa:

*“Hii ndiyo Jahannamu mliyokuwa mkiahidiwa! Ingieni humo leo kwa yale mliyokuwa mkiyakanusha.”*

**Qur'an 36:63-64**





makafiri kuna adhabu mbaya kabisa:

*“Hakika Jahannamu ilikuwa ni mtego, kwa wapotovu, mahali pa kurejea. Watakaa humo kwa zama nyingi (zisizo na mwisho). Hawataonja humo baridi wala kinywaji isipokuwa maji ya moto na usaha wa vidonda – malipo yanayostahiki (kwa matendo yao maovu)! Hakika wao walikuwa hawatarajii kuhesabiwa, na walizikanusha Ishara Zetu kwa ukali. Na kila kitu tumekiandika katika Kitabu. ‘Basi onjeni adhabu, wala hatutawaongeza chochote isipokuwa mateso!’”*

Qur'an 78:21-30

## HITIMISHO

*“Ewe mwanadamu! Ni nini kilichokudanganya kuhusu Mola wako Mkarimu? Ambaye Amekuumba, Akakuweka sawasawa, na Akakufanya kwa uwiano unaofaa. Katika sura yoyote Aliyopenda, Amekufanya. Sivyo! Bali nyinyi mnakadhibisha Malipo (malipo ya mema na adhabu ya maovu Siku ya Hukumu).”*

Qur'an 82:6-9

Kifo ni jambo lisiloepukika. Madhumuni yetu ya maisha ni kumuabudu Allah peke Yake, kutenda matendo mema, na kuepuka yote yaliyokatazwa. Hatima yetu inaamuliwa kulingana na matendo yetu ya sasa, hivyo tunaweza kutumia fursa tulizopewa duniani kuhakikisha tunapata nafasi ya milele Peponi, au tukaipoteza na kujihukumu wenyewe kuingia Motoni.

*“Hakika wacha Mungu watakuwa katika neema, na hakika waovu watakuwa katika Moto wa Jahannamu.”*







Qur'an 82:13-14

**HOTLINE**  
**+971 56 204 2045**  
  
**islamicicdx**  
 islamicic.com    info@islamicic.com    +971 4 355 5223

SCAN QR CODE FOR E-VERSION OF FLYER

icdx.com/swahili

CONTENTS



سبيلك للسلام  
Your Path To Peace..  
**FREE COPY**



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

# UPAGANI

## Kwa mtazamo wa ki-Islamu

SWAHILI [10/10]

الإحاد

*Tutawaonyesha (ukweli wa) maneno Yetu haya katika nchi za mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli . Je! Haikutoshi kwa Mola wako kuwa Yeye ni Mjuzi wa kila kitu?"*

(Qur'an 41:53)








PART OF



icelibrary.com | islamicic.com



دائرة الشؤون الإسلامية والعمل الخيري | Islamic Affairs & Charitable Activities Department  
(2017/139)



Makala haya yanabainisha mtazamo wa ki-Islamu katika kumuamini Allâh (Aliyetukuka.) Yanafafanua jinsi Allâh Anavyozibainisha alama za kuwepo Kwake kwa mwanadamu, sawa katika njia zote mbili, uumbaji Wake wa asili, na kwa uteremsho Wake wa Wahyi, na anabainisha maswali ya kawaida kwa wasiomuamini Allâh (wapagani)

Hakika Allâh (Aliyetukuka). Anatulingania sisi kuamini kuwepo Kwake kwa kutumia alama Zake, na Ametukalifisha sisi kwa kuamiliana nazo na kuzizingatia ili tufikie katika kumtambua Yeye na lengo Alilotuumbia, wameamini baadhi ya watu kwa kuona kwao alama zilizowazunguka na utendakazi wake, na wamekufuru baadhi yao kwa wanayoyaona katika mazingira yao na wanayoyahisi katika maumbile. Na Allâh (Aliyetukuka) amewaumba viumbe wake juu ya Imani, isipokuwa haya matayarisho ya ki-maumbile yawezekana kuitilia nguvu na kuitakasa kama inavyowezekana kuiharibu na kuichafua.

*Isipokuwa kwa uhakika katika jambo muhimu la kufahamu ni kwamba Allâh anamuongoza mtu aliye mkweli na mwenye ikhlâs ili aifikie uongofu Wake, na anampoteza aliyechagua kufuata matamaniao ya nafsi yake na anayemkanusha Yeye na Uongofu wake. Amesema Allâh (Aliyetukuka): “na anawaongoza wanaoelekea kwake”*

(Qur'an 13:27)

Na hili linahitajika juu ya mtu mwenye kukanusha kuwepo kwa Allâh (Aliyetukuka). Na akautenga mbali msimamo wa uwezekano wa kuwepo kwa Allâh (Aliyetukuka) usiwe ni wenye kuzingatiwa, na jambo la fedheha. Na bila ya kupatikana ombi hili la ufahamu mpana wa uhakika kwa mwenye kutafuta haki, hakuna awezae kufikia katika Imani ya kweli hata akiwa ni mjuzi zaidi na aliye na uhodari mkubwa miongoni mwa watu.

*Na ni muhimu vilevile kutaja kwamba kupatikaniwaa sababu za kuhitalifana baina ya Uislamu na Ukristo, katika kumfahamu Allâh, makosa mengi yanayotupiwa Ukristo hayahusiani na Uislamu.*

Kwa hakika Allâh ametangulia kutuonya kuhusu ukweli wa jambo hilo yakwamba wale wenye kufanya kiburi na alama Zake watapata malipo wanayostahiki kutokana na ukafiri wao.

Kwahivyo, twatumai yakwamba watafaidika wale walio wakweli, na waliofunguka akili zao wenye kutafuta ukweli kutokana na uhakika wa habari hizi, ambazo zitasaidia katika kupata kumfahamu Allâh .








# Sababu za kuamini

Zifuatazo ni sababu tatu za kiakili za kuamini kuwepo kwa Mumbaji.

## 1. Kuanza kwa viumbe

Hoja ya kwanza yenye kuashiria kuwepo kwa Muumba yafungamana na kuanza kwa viumbe.

Hebu fikiria uwe katika jangwa na uokote saa. Twajua kuwa saa imeundwa kwa kioo, plastiki na chuma. Kioo kinatokana na mchanga, na plastiki yatokana na mafuta, na chuma kimetoka chini ya ardhi. Madini yote hayo yanapatikana jangwani. Jee utaamini kuwa saa ilijitengeza yenyewe?




Jua limeng'ara, na upepo uka vuma, na radi ikapiga, na chemchem ya mafuta ikaja yenyewe juu na kuchanganyikana na mchanga na chuma na zaidi mamilion ya miaka saa ikajiunda yenyewe kibahati au hivihivi tu?

Kulingana na elimu ya sayansi ya wakati huu, ulimwengu una mipaka na una mwanzo. Ulimwengu umekuja kutoka wapi? Akili ya binadamu na uzoefu wake unatuambia chochote kilicho anza hakiwezi kuanza bila kutokana na kitu, wala haiwezekani kujiumba chenyewe. Kwahivyo kutokana na tafsiri ya wengi wenye kutumia akili ni kwamba yuko

muumbaji aliyeuumba huu ulimwengu. Huyu “Muumbaji” ni lazima awe ni Muweza na ni Mjuzi kwa kuwa yeye ndiye aliyeuumba huu ulimwengu na akaweka nidhamu za kuuendesha huu ulimwengu. Na pia twaweza kuamini kuwa huyu Muumbaji yeye hayumo kwenye nidhamu ya wakati au ya pahali kwani hayo yamepatikana pale ulipoumbwa ulimwengu. Sifa hizi zote ni zenye kuleta maumbile ya ufahamu wa kimsingi kuhusiana na Allâh. Kwamba Yeye ndie Muumbaji wa ulimwengu.

Na huenda wakaulizana baadhi: “Basi ni nani aliyemuumba Allâh?

Allâh, ndie Muumbaji, Yuko tafauti na viumbe vyake. Allâh ni wa tangu na tangu, Yeye daima yupo na kuwepo kwake hakuna mwanzo; Kwahivyo suala la kuwa ni nani aliyemuumba Allâh haliingi akilini.



## 2. Ukamilifu kuumbwa ulimwengu

Ushahidi wa pili wenye kuashiria ya kuwepo kwa Muumbaji, Mjuzi ni nidhamu na usawa uliokamilika mfano ni ulimwengu ulio na mambo mengi.

Jee yawezekana ulimwengu huu mkubwa wenye mambo mengi unao kwenda kwa nidhamu uwe hivihivi bila chochote wala muangaliaji?

Viumbe vingi katika ulimwengu vinaonyesha waziwazi kuwa vimetengezwa kutilia nguvu uhai, kama umbali wa jua kutoka ardhi; unene na kina cha ardhi; kasi ya mzunguko wa ardhi; asilimia ya pumzi katika hewa; na hata sehemu ya juu ya ardhi. Lau vipimo vya vitu hivi vingekuwa tafauti na vilivyo leo basi hapangelikuwa na uhai.

Hivyo hivyo saa ina mjuzi wake aliye itengeza ili isipoteze wakati, hivyo hivyo dunia ina mjuzi wake aliyeitengeza ili upate kwenda sawa mzunguko wake wa jua. Jee hili laweza kufanyika lenyewe tu?

Na tunapo angalia, nidhamu na kanuni zilizosawa ndani yetu sisi wenyewe na ulimwenguni kote, jee haingii akilini kuwa yuko aliyeweka nidhamu hizi? Na tafsiri iliyobora ya hili ni kuwa yuko aliyeweka nidhamu na huko ndiko kupatikaniwa kwa Allâh. Aliye Mmoja – aliyeweka nidhamu hizi.

Na ifahamike yakwamba Uislamu unahimiza utafiti wa kielimu na unahimiza kuzingatia. Kwa namna yakuwa ilmu ina mchango katika kutusaidia kutusifia baadhi ya nidhamu zilizowekwa na Allâh katika viumbe vyake, na katika kuzingatia upeo wa nguvu Zake na hikma Zake, kuendelea katika uvumbuzi wa kisayansi, kama chombo chochote au taratibu yoyote tuionayo katika ulimwengu huu kama vile mzunguko wa maji au gravity – ni alama ya kuonyesha yakwamba yuko muumbaji na aliyeupanga huu ulimwengu.

### 3. Ufunuo kutoka kwa Allâh

Ushahidi wa tatu ni ufunuo wa uhakika ambao Allâh Aliutumiliza kwa wanadamu kama alama miongoni mwa alama za kuwepo Kwake.

Moja katika makusudio ya Qur'an ni kuwalingania watu kufikiria na kuzingatia katika viumbe vya Allâh kama njia ya kukupelekea kumuamini Yeye. Na katika Qur'an , Allâh Atutaka tuzindukane kutokana na miujiza yake katika viumbe vyake kwenye ulimwengu wenye mambo mengi na katika nafsi zetu, ambazo zinatosheliza kutuonyesha yakwamba sisi tumeumbwa na Allâh Al-Hakîm, kwa mfano huo, amesema Allâh Aliyetukuka:

*Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na katika kuandamizana usiku na mchana, na katika mwendo wa vyombo ambavyo hupita katika bahari kwa kuchukua vitu viwafanyavyo watu, na (katika kumiminika maji aliyoyateremsha Allâh kutoka mawinguni, na kwa maji hayo akaihuwisha ardhi baada ya kufa kwake, na akaeneza humu ulimwengu kwa ajili ya maji hayo kila ya aina ya wanyama; na katika mabadiliko ya upepo, na mawingu yanayo amrishwa kupita baina ya mawingu na ardhi; bila ya shaka katika haya) zimo ishara kwa watu wenye akili (kuwa yuko Allâh na ni Mmoja)."*

**Qur'an 2:164**








Na zaidi ya hivyo, ziko aya zilizo waziwazi zenye kuonyesha kuwa Qur'an ni maneno ya Allâh Aliyetukuka, tutataja baadhi yake:

#### Qur'an Tukufu

- Allâh anaepukana na makosa na kuchanganyikiwa.
- Ameyahifadhi maneno Yake kama Alivyoyateremsha, ameteremsha ufunuo kwa lugha ya kiarabu, kinyume na lugha nyenginezo za vitabu vilivyopita.
- Ujumbe wa Qur'an ukowazi na ni mwepesi, humpelekea mwenye akili kumuamini Allâh Aliyetukuka.
- Qur'an imeteremshwa zaidi ya miaka 1400. Ambayo ndani yake muna hakika nyingi za kielimu ambazo zilikuwa hazijulikani wakati ilipoteremshwa ambazo zimetimia uvumbuzi wake hivi karibuni kupitia elimu. Na mfano wa hayo: maji ambayo ni asili ya kila kilichoko hai (Qur'an 21:30); kuumbwa kwa ulimwengu (Qur'an 51:47) na kuumbwa kwa usiku na mchana na jua na mwezi kila kimoja kinaogelea katika anga yake (Qur'an 21: 33)
- Katika Qur'an kuna hakika nyingi za kihistoria ambazo hazikuwa maarufu kwa watu wa wakati ilipoteremka, mbali na utabiri mwingi uliotokea baada yake ukiwa ni kweli.
- Qur'an iliteremshwa kwa Mtume (swala na salamu zimfikie) ambaye alikuwa hajui kusoma kilichoandikwa, na ina mfumo wa aina yake katika lugha yake, na hilo ni jambo maaruf ulimwengu kwa kuzingatia kilele cha ufasaha wa lugha ya kiarabu na uzuri wa ki-lugha.
- Na baada ya tafsiri nyingi za kimantiki pande mbalimbali za kipekee na miujiza ya Qur'an ni kwamba yatoka kwa Allâh .

*Qur'an inahifadhiwa kutoka jalada mpaka jalada na mamilioni ya Waislamu.*

*Qur'an inaathiri sana watu, ambayo athari yake hiyo hakuna mwenye kuihisi ispokuwa aliyeonja utamu wa imani.*



# Maswali kuhusu Allâh

## Kwa nini Allâh Alitumbua?

Yawezekana kila mmoja wetu kutambua yakwamba viungo vya mwili, kama macho mawili, masikio mawili, bongo na moyo vina malengo maalum katika kuwepo kwake, jee mtu kwa umbile lake kamili atakuwa hana lengo aliloumbiwa nalo?

Allâh, Al-Hakîm Aliyetukuka hakutuumba sisi bila ya lengo au kwa ajili ya kutekeleza mahitajio yetu ya kimsingi na matamano yetu ya kula na kunywa na kuoia kwetu peke yake, sisi tuna lengo maalum, na upeo wa juu, nayo ni kuamini kuwepo kwa Allâh Mtukufu na kumuabudu Yeye peke Yake, na maisha haya tunayoishi ni mtihani kama alivyo yasifu Allâh Mtukufu, kila mtu atatahiniwa kwa uchaguzi wake wa kumuamini Allâh na kufuata uongofu Wake, Amesema Allâh Aliyetukuka

*“Kwa hakika Tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika: (ya mwanamume na mwanamke), ili Tumfanyie mtihani (kwa amri Zetu na makatazo Yetu) kwa hivyo Tukamfanya ni mwenye kusikia (na) mwenye kuona. Hakika Sisi Tumemuongoza, (tumem’bainishia) njia (zote mbili hizi, kuwa hii ndiyo ya kheri na hii ndio ya shari). Basi (mwenyewe tena) atakuwa mwenye shukurani au awe mwenye kukufuru, (kukanusha).*

Qur’ân 76:2-3

Kwa watu wengi, si jambo la kimsingi kwa uhakika kumuamini Allâh, lakini ni ile athari iliofungamana na kumuamini Yeye. Kwani hilo linamaanisha kwa mtu kuwa atahisabiwa na kuhukumiwa juu ya vitendo vyake, na huenda hilo likawa halikulekeana na mwenendo wa maisha yake anayotaka kuishi mtu huyu. Na kwa hivyo, hakika mtihani kwa maisha haya yanafungamana na kufuata uongofu wa Allâh, na kumnyenyekea Yeye, kinyume na matamano yetu na kiburi na kujiona kwetu.

## Jee Allâh anahaja yoyote katika mitihani Anayotupa?

Allâh Aliyetukuka hana haja na kitu chochote – na Yeye hana haja ya kitu chochote kwa viumbe na hata mtihani wa mtu yeyote.








Hakika Allâh Aliyetukuka haimnufaishi Yeye imani yetu, wala hadhuriki na ukafiri wetu. Bali hakika malipo kwa hikma Yake iliyoenea ni kwamba Yeye ametuumba sisi na kwa neema Zake akatupa sisi fursa ya kumjua Yeye, na Yeye Aliyetakasika anajua yatakayo kuwa, na jambo la kuzingatia ni maisha yetu na uzoefu wetu na uamuzi wetu wala si kwamba Allâh Anahaja ya mitihani au la.






## Jee kwa hakika tunayo khiari?

Kwa hakika Allâh Aliyetukuka ajua khiari zetu haimanishi kwamba sisi hatukhiarishwi katika kufanya. Pamoja na kwamba Allâh analolitaka kwa watu wamuamini Yeye, ispokuwa ni kwamba Allâh hamlazimishi hata mmoja katika hilo. Lau angalitaka Allâh angeliwaongoza watu wote, kwani Yeye ni muweza kila kitu. Lakini kwa hikma Yake, lakini Ametuumba na akatujaali uwezo wa kukhiari, na akajaalia ya kwamba tutahisabiwa kwa yale tulio khiari sisi wenyewe. Wala si dharura kwa Allâh Aliyetukuka kuridhia kila alilikubali kuwa kwetu sisi au dhidi yetu.

## Kwa nini hatuwezi kumuona Allâh ?

Kwa hikma ya Allâh Aliyetukuka, amechagua tumjue Yeye kwa alama Zake na athari ya utenda kazi wake, na haya ndio malipo ya mtihani wetu katika maisha haya.





Na tumebebishwa amana ya kuchagua baina ya kheri na shari, kwa kutumia uwezo aliotuneemesha Yeye ili tupate kumuamini Yeye, na hili linamaana ya kuwa wale walio wa kweli watakaofikia uwongofu na wakazingatia katika uumbaji wa mbingu na ardhi ndio watakao muamini Yeye.

**Kwanini kukapatikana shari katika ulimwengu huu?**

Kwa hakika watu wametafautiana, na njia ya mtihani wao pia umetofautiana, haina maana yakuwa kwa hilo Mola hayupo wala halipingani na uwezo Wake kwa ujumla.

Kwa hivyo kheri na shari ambayo Allâh ameijaalia itokee ni mtihani kwetu katika haya maisha tunayoishi. Hatuwezi kuzuia yenye kutokezea kwetu, lakini twaweza kujituliza katika vitendo vyetu tunapo yaelekea hayo matukio, na hayo ndiyo tutakayohukumikiwa nayo na Allâh aliyetukuka. Hakika huu ulimwengu ni wa kupita na unao zunguka, na akhera ambayo ni ya kuthubutu na kudumu kila mmoja atalipwa kwa aliyo yachuma, na atapata hadhi yake kutokana amali zake nyingi na kubwa zaidi kuliko zilivyokuwa.

**Kwa nini Allâh Atawaadhibu watu?**

Haiwezekani mtu kupinga ufahamu wa adhabu, chenye kuzingatiwa ni kuwa ni kitu cha dharura cha kuhakikisha uadilfu. Hakika Allâh Ametuumba na akatupa neema ya uwezo wa kuchagua, na kwa msingi huo tutahisabiwa vitendo vyetu.

Wale walio wakweli katika kumtwi'i Allâh Aliyetukuka watapata rehema Zake, na wataingizwa peponi. Na wale ambao wameghafilika na makusudio waliyo umbiwa, na wakapinga kuwepo kwa Mola wao, hakika wao wamechagua njia yao, na watahisabiwa kwa kuifuata kwa hiyo njia yao. Hakika Allâh Aliyetukuka hakuumba viumbe kuwaadhibu, na kwa hakika alitaka kuwasahilishia wao mambo yao na awaongoze kwa tabia njema. Na kwa hakika Allâh Aliyetukuka anajua yakuwa uamuzi wetu hauna maana ya kuwa tumetenzwa nguvu wala hautatufanya sisi tusihisabiwe kwa vitendo vyetu.

Hakika Uislamu ni dini ya vitendo, unahimiza juu ya kuwa na mizani katika vitendo baina matarajio ya rehema ya Allâh na hofu ya adhabu Yake, na hayo yote yanahitajika kwa dharura ya maisha yalio mazuri. Kwani hakika Allâh Aliyetukuka, Yeye ni Rahimu, naye ni muadilifu katika hukmu Zake. Ikiwa kutakuwa hakuna siku ya kiyama, hilo litakuwa lapingana na uadilifu wa Allâh Aliyetukuka, na maisha yatakuwa hayana uadilifu.

**Hitimisho**

Jee sisi tuko hapa ulimwenguni kwa miaka 80 au karibu ya hapo? Ili mambo yeshe?! Au yako maisha mengine?

Jee sisi ni masokwe walio endelea ambao hawana malengo katika maisha? Jee sisi ni viumbe waki mada tulioumbwa kwa mahitaji ya kimada peke yake? Au sisi pia tuna mahitaji ya kiroho?

Kwa wale wlio wa kweli na bado hawaja amua kuhusu kuwepo kwa Allâh, naswiha yetu kwao ni kuomba Allâh kikweli kwa kusema:

*“Ewe Allâh ikiwa uko basi niongoze” na huenda ukashangaa kwa matokeo yake!*

**HOTLINE**  
 +971 56 204 2045  
 islamicicdx

islamicic.com @ info@islamicic.com +971 4 355 5223



مركز المعلومات الإسلامي  
Islamic Information Center

لتعريف بالإسلام

Part of the



# ISLAMIC e-LIBRARY

Learn more about Islam with our informative and educational materials, translated to over 50+ languages



Quran



Flyers



Books

[iicdxb.com/flyers](http://iicdxb.com/flyers)

@islamicicdxb

